KISWAHILI

5

# SANIFU KWA SHULE ZA SEKONDARI

KITABU CHA MWANAFUNZI
KIDATO CHA TANO

TAN PRINTS

# YALIYOMO


YALIYOMO iii

UTANGULIZI iv

SURA YA KWANZA : FASIHI. 1

SURA YA PILI : TAMATHALI ZA USEMI 23

SURA YA TATU : MATUMIZI YA LUGHA 30

SURA YA NNE : MNYAMBULIKO WA VITENZI 40

SURA YA TANO : UHAKIKI 45

SURA YA SITA : UFUPISHO 53

SURA YA SABA : HOTUBA 60

SURA YA NANE : AINA ZA TUNGO 64

SURA YA TISA : SARUFI MIUNDO 70

SURA YA KUMI : UTUNGAJI 75

# UTANGULIZI

Hiki ni kitabu kipya kilichoandaliwa kwa ajili ya wanafunzi na waalimu wa Kiswahili kidato cha tano katika shule za sekondari.Ni cha kukidhi haja ya muhtasari wa sekondari nchini Rwanda.Hii ina maana kwamba maelezo yote kuhusu somo hili yatakayotolewa humu yatakuwa ni yale yanayolingana na kidato hiki.

Kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano, kina ndani mwake masomo yanayotarajiwa kufundishwa wanafunzi wa Kiswahili kidato husika, ambayo ni pamoja na : Fasihi, tamathali za usemi, matumizi ya lugha ya Kiswahili, mnyambuliko wa vitenzi, uhakiki, ufupisho, hotuba, aina za tungo, kupambanua na kuchambua tungo, na utungaji wa barua mbalimbali. Kitabu hiki kimeandikwa na Bwana **NIYIRORA Emmanuel** na **NDAYAMBAJE Ladislas**, kutoka Chuo Kikuu cha Elimu cha Kigali (KIE). Kitabu hiki kitawasaidia wanafunzi kujua lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya kibantu na iliyopiga hatua kimatumizi, kimsamiati, na yenye kutumiwa na jamii mbalimbali barani Afrika na ulimwengu kwa ujumla. Kwa sababu Rwanda imeingia katika Jumuia ya Afrika Mashariki, ni lazima Wanyarwanda wote wawe na ujuzi wa lugha hii muhimu. Katika kitabu hiki mwanafunzi anapatiwa maelezo, mifano na mazoezi kuhusu mada inayofundishwa ili kuieleza vyema.

Tunawatakia mafanikio mema watu wote watakaosoma na watakaotumia kitabu hiki.

NIYIRORA Emmanuel

NDAYAMBAJE Ladislas,

Juni, 2012

# SURA YA KWANZA : FASIHI.

## 1.1. DHANA YA FASIHI

Fasihi ni aina ya sanaa ambayo wasanii wake huonyesha ustadi wao katika kutumia maneno kisanaa ili kuwasilisha ujumbe wao kwa wasomaji/jamii iliyonuiwa.Hii ndiyo tofauti kubwa baina ya fasihi na sanaa nyingine kama uchoraji wa picha, uigizaji wa densi, utungaji na uimbaji wa ngoma au mziki, usukaji mikeka, uchongaji wa vinyagona kadhalika ambamo nguzomuhimu si lugha bali ni vifaa vitumikavyo.

Fasihi hutumia lugha kufafanulia tabia za watu na athari zake huku ikituzindua ili tuone uzuri au ubaya wa jambo au tabia fulani kama vile wizi, wivu, tamaa na kadhalika.

Fasihi hushughulikia ulimwengu halisi na mambo yale yale yanayotuzunguka. Tunapoyachambua mambo hayo, tunaona kuwa yanatukia katika mazingira yetu pia na yanatupa mafunzo muhimu maishani.

## 1.2. TANZU ZA FASIHI :

Ingawa fasihi ni moja, inazo tanzu mbili muhimu : fasihi andishi na fasihi simulizi. Fasihi andishi ni ile iliyoandikwa vitabuni, vipengele vyake vikiwa riwaya, hadithi fupi, tamthiliya na ushairi. Fasihi simulizi nayo ni ile ambayo inapitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia neno la mdomo.

Fasihi hizi mbili zina uhusiano mkubwa. Kwanza, katika miaka ya karibuni kumekuwa na juhudi ya kuzihifadhi ngano, nyimbo, ushairi, methali na kadhalika za jamii tofauti katika vitabu. Pili, fasihi simulizi imechangia kwanjia kubwa ufanisi wa fasihi andishi. Asilimia kubwa ya fasihi andishi ina mizizi yake katika hadithi, mashairi na kadhalika ambayo waandishi walipitia kama watoto wadogo. Fasihi ni kioo cha jamii au mwavuli mkubwa unaohifadhi mila na desturi za jamii fulani kwani jamii yoyote iwayo hujitambulisha kwa fasihi yake.

Katika sura hii tutaiangalia fasihi kwa ujumla, tukigusia vipengele vya kawaida baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Tanzu za fasihi simulizi na zile za fasihi andishi ni hizi zifuatazo :

- Vitendawili
- Hadithi
- Methali
- Nahau
- Nyimbo
- Tamathali za usemi

## 1.2.1.VITENDAWILI

### I.2.1.1.DHANA YA VITENDAWILI.

Vitendawili ni mafumbo ya maneno ambapo vitu na hali ya kawaida hurejelewa kipicha ili tuweze kufumbua kinachosemwa hasa.Katika kuvichambua vitendawili, mwanafunzi anatakiwa kuchunguza mambo kadhaa :

a) Muundo wa kitendawili-hapa utatazama umbo kwa ujumla na kujiuliza : sehemu za kitendawili zinahusiana vipi na jibu?

b) Uhusiano wa kimantiki baina ya kinachoulizwa na jibu linalotarajiwa.

c) Matumizi ya lugha ya picha katika kitendawili.

d) Jinsi lugha iliyotumika kwenye kitendawili inavyofaulisha ujumbe unaokusudiwa.

e) Maneno na sauti zisizokuwa maneno zilizotumika(kwa mfano Huko "ng′ona huku ng′o"ambayo jibu lake ni giza).

f) Umbo la kitendawili.Je, kitenndawili ni swali?Kifungu ambacho Hakijakamilika? Kimeandikwa kinathari au kishairi?Kama wimbo au maghani?

### 1.2.1.2.UAINISHAJI WA VITENDAWILI

Aghalabu vitendawili huainishwa ifuatavyo :

- Vitendawili vinavyohusu watu.
- Vitendawili vinavyohusu vyombo vya kitamaduni.

- Vitendawili vinavyohusu mimea.
- Vitendawili vinavyohusu maumbile.
- Vitendawili vinavyohusu ndege.
- Vitendawili vinavyohusu sehemu za mwili.
- Vitendawili vinavyoeleza hali fulani.
- Vitendawili vinavyouliza maswali.
- Vitendawili vinavyotolewa kwa njia ya mfululizo wa mambo.
- Vitendawili rahisi.
- Vitendawili vigumu.

*Vigezo muhimu vya kumwongoza mwanafunzi kuviainisha vitendawili ni kama vifuatavyo :*

- Urahisi au ugumu wa kitendawili.
- Muundo na mtindo wa kitendawili.
- Vitu/hali/vyombo vinavyorejelewa katika kitendawili.

### 1.2.1.3.MTINDO WA UTEGAJI WA VITENDAWILI.

Jamii mbalimbali zina fomula tofauti za kutanguliza vitendawili.

Kwa mfano, Wagriama wataanza hivi :

***Msimulizi/mtegaji*** : Chandoni!

***Hadhira/mteguzi*** : Ndekeha!

Kisha ***msimulizi*** atasema : "Kitendawili changu ni : ……".

Wakamba nao, huanza vitendawili hivi :

***Msimulizi/mtegaji*** : Kwatai ndai (Chukua kitendawili)

***Hadhira/mteguzi*** : Nakwata (Nimechukua).

Wengine nao, kama Wanyarwanda, wanasema :

***Mtegaji*** : Kitendawili !

***Mteguzi :*** Tega !

Katika jamii nyingi msimulizi hudai apewe zawadi ambayo hutofautiana toka jamii moja hadi nyingine.Katika baadhi ya jamii inaweza kuwa msichana wa kuoa, mji au mnyama.Je, jamii yako hudai zawadi gani wakati wa utegaji wa vitendawili?

### 1.2.1.4.BAADHI YA VITENDAWILI.

- Ninampiga msichana wangu kila siku lakini hasikii=***Kinu.***
- Chakula kikuu cha mtoto=***Usingizi***
- Kipo lakini hukioni=***Kisogo***
- Kila mtu anapitia mlango huo=***Kifo***
- Zilikaa, zinakaa na zitakaa mbilimbili=***Mboni***
- Yeye hazungumzi**=*Ulimi***
- Wanihisi lakini hunioni=***Upepo***
- Yamkumbapo harudi tena**=*Mauti***
- Wanangu wengi hawahesabiki=***Nywele***
- Kwa bi Liwali kumetanda wingu jeusi=*Nuksi/bahati**mbaya***.
- Wanameza watu jua linapokuchwa (Kuchwa=zama jua)=***Nyumba.***
- Watoto wangu wote nimewavika kofia nyekundu=***Jogoo***
- Viti kumi nyumbani, tisa vyakatika lakini kimoja hakikatiki=***Moto***
- Ukiingia nyumbani mwako hutoki tena=***Kaburini***
- Upande wowote umjiao atakuona=***Kinyonga***
- Tantarapa mlango wa chuma hauna huruma=***Bunduki***
- Tunamsikia lakini hatumwoni=***Sauti***

- Wasichana wangu wawili wapepeta mpunga mlimani=***Matiti***
- Kila kitu chageuka isipokuwa mimi=***kabila***
- Mti wangu nikiukata haukatiki=***Maji***
- Tatu tatu mpaka pwani=***Mafiga***
- Akizungumza kila mtu hubabaika=***Radi***
- Taa yangu yazagaa(yaenea)ulimwengu mzima=***Mwezi***
- Ajenga ingawa hana mikono=***Nyuni/ndege***
- Rafiki yangu anatembea kwa tumbo= ***Nyoka***.
- Rafiki yangu ana mguu mmoja=***Uyoga***
- Ni mfalme lakini hana raia wala askari=***Simba***
- Ninaona juu ya mti=***Twiga***
- Ndege wengi waangaza baharini=***Nyota***
- Nyumba yangu haikosi maji=***Kinywa***
- Ni la kupendeza lakini halikai=***Ua***
- Nikiita "baba "huitika" baba"=***Mwangwi***
- Nakupa lakini mbona huachi kudai=***Tumbo***
- Nanywa mchuzi na nyama naitupa=***Muwa***
- Guu la tembo huenda kwa madaha=***Matende***
- Ni saa ambayo haijasimamia tangu kutiwa ufunguo=***Moyo***
- Akivaa nguo hapendezi, akiwa uchi yuapendeza mno=***Ndizi***
- Mshale unaowalenga wote=***Jua***
- Kitanda changu cha dhahabu nikilalia siamki tena=***Jeneza***

## MAZOEZI

Tegua vitendawili hivi vifuatavyo :

1. Amezaliwa Ali, amekufa Ali na amerudi Ali
2. Anachora bila kutumia akili
3. Anatuona lakini sisi hatumuoni
4. Askari wamekaa pembeni na mfalme yu katikati
5. Chakula kikuu cha mtoto
6. Yamkumbapo harudi tena
7. Upande wowote umjiaon atakuona
8. Nanywa mchuzi na nyama naitupa
9. Ninaona juu ya mti
10. Mshale unaowalenga wote

### 1.2.2. HADITHI

Kuna aina kuu mbili za hadithi ambazo ni pamoja na :

- Hadithi fupi
- Riwaya

#### 1.2.2.1.HADITHI FUPI

Hadithi fupi ni mojawapo ya tanzu za fasihi andishi.Hadidhi fupi inaweza kufafanuliwa kwa njia zifuatazo : Ni masimulizi ya kubuni yaliyoandikwa juu ya tajiriba fulani ya maisha.Sifa yake kuu ni ufupi wake ambao ni tofauti na ufupisho wa riwaya.

***Mfano wa hadithi fupi*** :

## MOSE AVUNJA MWIKO

Mose alikuwa tofauti sana na watoto wengine pale kijijini kwao.Mose alimsaidia mama yake kwa kazi za nyumbani, kinyume na wavulana wengine.Ungemkuta nyumbani

akiosha vyombo, akifagia nyumba, akipasua kuni, akipika na kwenda mtoni kuleta maji. Alipojitwika mtungi juu ya kata utosini mwake, wanakijiji walishangazwa na uhodari wake wa kubeba maji kichwani.Alifanya hivyohivyo alipobeba mzigo wa kuni ama kikapu cha mavuno ya shambani.

Wavulana wenzake walimcheka sana.Kwa hakika, siku moja walimvua kaptura kwa nguvu, ili kuhakikisha kama kweli alikuwa mvulana.Babake Mose alikuwa pia akimsaidia mkewe katika kazi za nyumbani.Wanakijiji walidai kuwa baba Mose alikuwa 'amekaliwa na mkewe' na ndoyo maana alikuwa akifua nguo na kupika mkewe alipojifungua.Wanakijiji hawakuamini macho yao walipomwonana Baba Mose akianika nepi kwenye kamba baada ya kuzifua.

Siku moja wazee wane wa kijiji walimwendea Baba Mose na kumwambia : "Kijana, tunataka kukufahamisha kwamba mambo unayoyafanya hayafai kufanywa na mwanaume. Umeonekana jikoni mara kadhaa ukipika.Hata nguo za mkeo unamfulia.Unatutia aibu sana sisi wazee wa kijiji.Hata Mose, mtoto wako amekuwa na tabia sawa kabisa na yako…"

"Eeh, "Baba Mose alianza "maisha ya siku hizi si kama yale ya zama za babu zetu.Nyakati zinaenda zikibadilika.Lazima tukubali kwamba mahali pa mwanamke siyo jikoni tena;babu yangu alikuwa na wanawake wawili.Aliporudi kutoka ulevini, alijiangusha kwenye lango la mji wake.Wake zake walikuja mbio na kumbeba.Mwanamume wa kisasa akijaribu tamthiliya ya aina hiyo, hatairudia tena!Atalala nje, kwa hivyo wazee, najua ninachofanya. Msiniletee mafunzo yasiyoafiki usasa.Ulimwengu wa leo sio sawa na ule wa zama zenu."

"Haya kijana, "akasema mzee wa pili.Haidhuru maadam imeonekana mmekubali kutawaliwa.Basi vueni suruali mvae marinda ya wake zenu!"

"Wazee"Baba Mose alimkatiza, "Tofauti kati ya kizazi chenu na chetu ni kubwa kama ardhi na mbingu.Hatuwezi kuelewana.Yafaa tuhesimiane.Haifai kurushiana cheche za matusi zitakazotupelekea kuvunjiana heshima.Niacheni niendelee kuuma jongoo kwa meno."

Mose naye alipokua kidogo, alitatanika mpaka akaenda kuomba mawaidha kwa mwalimu mshauri shuleni kwao."Usijali, Mose, kutukanwa na kuchekwa na wavulana wenzako kwa sababu ya kumsaidia mama yako.Utakapooa, utaishi kwa furaha na mkeo.Hutamchukua mkeo kama mpishi na mzaaji, bali nyinyi wawili mtashirikiana kujenga familia yenu.Baba yako anastahili pongezi kwa kukuondoa katika ulimwengu wa ndoto, unaowadanganya wavulana wengi kuwa wao ni wanaume wanaofaa kuhudumiwa.Punde si punde wataupata

ukweli kwamba mwanamke mahali pake siyo jikoni tena, bali ni mwenzi na mshirika katika ujenzi wa familia na taifa kwa ujumla."

#### 1.2.2.2.RIWAYA

Riwaya ni hadithi ndefu iliyoandikwa kinathari.Aghalabu riwaya huandikwa kuhusu ukweli fulani wa maisha halisi.Utanzu huu ulizuka baada ya ngano na hadithi fupi kutokana na uchangamano wa maisha ya kisiasa, kitamaduni, kiuchumi katika historia ya mtu.

Sifa za uchangamano ni nzuri zaidi kuelezea maana ya riwaya.Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa riwaya ni kisa changamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kifani na kimaudhui

Hadithi fupi basi ni masimulizi yanayojikita katika kisa kimoja chenye uzito kimaana. Inambidi mwandishi wa hadithi fupi achague tu yale mambo ya lazima kuelezea.Hadithi fupi aghalabu huwa na mmhusika mkuu anayehusishwa na matukio makuu katika hadithi nzima.Wahusika huwa hawakukuzwa kikamilifu.Pia ufafanuzi wa mazingira (yaani muktadha kiwakati/kimahali/kimaumbile)huwa hayakukuzwa kikamilifu kama ilivyo katika riwaya.Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana maisha ya jamii.

***Mfano wa riwaya*** : Adili na nduguze(Shaaban Robert)

Mazoezi :

- Toa tofauti iliyopo baina ya hadithi fupi na riwaya.

### 1.2.3. METHALI

#### 1.2.3.1 Dhana ya methali

Methali ni semi fupi zenye maana fiche zinazokubalika na kutumiwa kufafanua ukweli na hekima ya jamii. Methali ni maarufu na zinaheshimiwa sana katika fasihi ya mwafrika.

Migogoro mingi ya kisiasa, kidini na kisheria aghlabu huhusihwa kwa kutumia methali. Mtu mwenye uwezo wa kutumia methali katika jamii ataibuka mshindi katika mjadala wowote.

**Mfano** : mijadala ya mahari ama posa ambapo lugha ya picha hutumiwa kwa wingi.

Methali hutumiwa pia katika utambaji wa hadithi, nyimbo na ushairi simulizi. Methali hutumiwa kuyatafakari na kuyapima maisha; kufunzia jumuia na kutawalia jamii na mazingira ya binadamu. Hutumika kama kioo ambacho jamii hujitazamia na kuwasilisha hekima ya wahenga tangu jadi. Methali hufafanua falsafa ya jamii na hekima ya wale wanaozitumia katika mazungumzo yao.

### 1.2.3.2. Baadhi ya methali za Kiswahili

**1. Adui wa mtu ni mtu**

Methali hii inasisitiza juu ya tahadhari. Binadamu ni lazima awe na tahadhari sana katika kuenenda na maisha; ni lazima ajihadhari na kiumbe hiki binadamu. Kama vile binadamu alivyo na uwezo mkubwa wa kuhisi ndivyo pia alivyo na uwezo mkubwa wa kuathiri. Mtu ni mtu lakini si kila mtu ana utu. Utu ni ubinadamu na ubinadamu ni mwenendo mwema kwa binadamu wengine.

Huo mwenendo mwema ni hiari na matakwa ya huyo mwenyewe. Hiari ni siri ya moyo. Kila mtu ana moyo wake. Kwa hiyo ana siri yake-hiyo aijuayo. Hiyo siri ya moyo wake yaweza kuwa njema au mbaya kwa mtu mwingine.Kwa hiyo kama vile ilivyo kweli kwamba adui yako aweza kuwa mwema wako ndivyo pia ilivyo kweli kwamba mwema wako aweza kuwa adui yako.

**2. Aliye kando haangukiwi na mti**

Hii ni methali nyingine ambayo yamtaka mwanadamu awe mwangalifu zaidi awe na tahadhali. Mti ni mti, na huumiza hasa umuangukiapo kiumbe kama binadamu. kwa hiyo binadamu akiuelewa huo udaifu wake na kama anataka kuishi maisha marefu zaidi, anawajibika kusimama kando ili mti usimuangukie.

Maana inayojitokeza hapa ni kwamba tusijitie katika mambo yasiyotuhusu au tusiyoyaweza. Ni lazima tuchunguze uhusiano na uwezo wetu kabla hatujaamua kujishirikisha katika mambo ya wenzetu. Kama tukibaini kwamba mambo hayo hayatuhusu, hatuyawezi au yanaweza yakatuletea madhara, basi tukae kando na tuwaachie wenyewe waendelee na mambo yao.

**3. Dawa ya moto ni moto**

Methali hii inajulikana sana kwa matumizi yake ya kila siku. Ni wazi kuwa ukitaka kukinga moto ambao unakuja basi nawe yakubidi uwashe moto. Hii hutumika kwenye vijiji vilivyo karibu na mapori. Maana ya methali hii hasa ni kwamba ubaya dawa yake ni ubaya vilevile. Yaani akufanyiaye mabaya basin awe mfanyie mabaya.Hivyo ubaya huo ukikutana aidha kutatokea namna Fulani ya usuluhisho. Tafsiri nyingine ya methali hii ni kwamba jambo lolote tukiona laenda kombo basi twatakiwa kuwahi kulitibu kabla halijawa baya.

**4. Fimbo ya jirani haiwezi kuua nyoka**

Methali hii inafanana na ile isemayo hamadi kibindoni. Huwezi kufanya jambo kwa kutegemea msaada kutoka sehemu nyingine (jirani). Jirani hawezi kutatua matatizo yako kama vile ambavyo wewe mwenyewe ungeyatatua. Jirani si wa kutegemea. Twahitajika kujitegemea wenyewe kuliko kutegemea wengine.

**5. Fimbo ya karibu ndio iuayo nyoka**

Ni kweli kwamba fimbo iliyo karibu ndiyo iwezayo kuua nyoka. Methali hii hutumiwa wakati unapoongelea jambo ambalo utatuzi wake watakikana haraka ama pengine bila kupata msaada sehemu nyingine. Msaada wowote, akiba yoyote ambayo ipo tayari kwa wakati unaotakiwa, ndio msaada pekee unaothaminiwa na kutambuliwa. Huwezi kutegemea kitu ambacho kiko mbali ama kukipata kwake kuna matatizo ikilinganishwa na kitu ambacho kipo tayari kihitajiwapo.

**6. Hata kiporo ni ugali**

Methali hii hutumiwa kwa kusema kuwa kwa kweli kula ni kula. Hakuna chakula ambacho hakina umuhimu. Chakula ni chakula hata kikiwa kiporo.

**7. Karamu mbili zilimshinda fisi kuzila**

Methali hii yatutahadharisha tusiwe wenye tamaa tama. Twaambiwa kuwa unapokuwa na haja ya jambo Fulani ukawa katika hali ya kutekeleza basi usirukie jambo jingine la aina ile ile maana waweza ukakosa huku na kule. Shika ulichoshika usifuate kile ambacho huna uhakika wa kukipata.

**8. Kauli nzuri ni bora kuliko mali**

Hakika kauli nzuri ni kweli kwamba ni bora kuliko utajiri. Hivyo ulimi kwa kweli kutokana na methali hii ni kitu cha kuchunga sana. Kabla hatujasema neno lolote twahitajiwa kuchuja na kuhariri yale tunayotegemea kusema kabla ya kusema, maana neno likishasemwa ni vigumu kufutika kwani lilishasikika.

**9. kifo hukaa kwenye mshipi**

Hapa mshipi umetumiwa kama kielelezo tu. Maana hasa ya methali hii ni kwamba binadamu tunapotembea tusijione kuwa ni kitu sana. Yatupasa kufahamu kuwa kila tunapotembea kifo kinatuzunguka.

**10. Kila mjinga ana manufaa yake**

Haiwezekani mtu awe mjinga moja kwa moja. Kuna siku anaweza kufanya mambo mazuri watu wakashangaa.Watu wengine huamini kuwa hakuna ujinga ambao ndani yake hauna welevu. Hivyo tusije tukawadharau watu kuwa ni wajinga na tukaamini hivyo moja kwa moja.Tukifanya hivyo tutakuwa tunafanya makosa.

**11. Kilichokatwa na shoka hupotea lakini kilichokatwa na mdomo hakipotei**

Ni wazi kwamba shoka linapokata daima hukata vitu ambavyo vyaweza kupotea. Kinachokatwa na mdomo aghlabu hakipotei, maanachaenda tumboni. Binadamu anapokata kitu kwa mdomo ni wazi kuwa baadaye hukila kitu hicho na kwamba kitamnufaisha katika kujenga, kulinda na kuhifadhi mwili. Methali hii yatushauli kuwa tufanye mambo yetu kwa dhamiri maana katika dhamiri kuna mafanikio. Tusifanye mambo juu juu tu ; bali kwa undani na dhati.

**12. Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake**

Si rahisi kufahamu kunguni wa kitanda usichokilalia wanauma kiasi gani. Hivyo anayelalia kitanda hicho ndiye anayefahamu kunguni wake.Kimatumizi methali hii inatueleza kuwa mtu hawezi kujua shida zinazompata mtu mwingine.Jambo lisilokuhusu ama kukupata huwezi kujua ubaya wake.

**13. Kuishi na ndugu ni kuvumiliana**

Methali hii inajieleza yenyewe. Ndugu wana tabia mbalimbali na nyingi ya tabia za ndugu ni kinyume cha vile ambavyo tungewatazamia wawe. Hivyo basi unapoamua kukaa na ndugu basi yakubidi uwe mvumilivu kwani vitendo vingine vyaweza kuwa vya kusikitisha na kutisha. Hivyo basi tunapoamua kukaa na ndugu lazima tuwe wavumilivu wa maovu yote ambayo watatufanyia.

**14. Macho mengi huona kuliko moja**

Uwingi daima ni bora maana una nguvu. Macho mawili ni bora zaidi kuliko bora. Umoja na ushirikiano ni ngao imara kabisa katika maisha. Katika umoja kuna ushirikiano na katika ushirikiano kuna mafanikio.

**15. Maji marefu muulize chura**

Chura kwa kawaida huishi majini. Twategemea kwamba ayajua vema mazingira yake. Kama ndivyo, basi yumkini afahamu urefu na ufupi wa maji. Yafaa kwa muogeleaji kutafuta ushauri wa chura hata kabla ya kuyazama maji. Ili tuufahamu undani na ukweli wa jambo yatubidi daima tufanye uchunguzi utakiwao. Njia mojawapo ya kuchunguza ni kuwauliza na kutaka ushauri wa hao wahusikanao na jambo hilo. Kuuliza ni kufahamu.

**Methali nyingine :**

- Maji yanayokuja kwa nguvu yape njia yapite
- Mali ni sawa na maua
- Maneno ya kaburini huishia kaburini
- Masikini halali mchana
- Maziwa ya ng′ombe wa kuazima yanywe huku ukisimama
- Kidole kimoja hakivunji chawa
- Kizuri chajiuza kibaya chajitembeza
- Apewaye ndiye aongezwaye
- Haraka haraka haina Baraka

- Mchagua jembe si mkulima
- Mwenye kovu usidhani kapoa
- Kutoa ni moyo usifikiri ni utajiri
- Bura yangu sibadili na rehani
- Chovya chovya humaliza buyu la asali
- Jungu kuu halikosi ukoko
- Chanda chema huvikwa pete
- Umleavyo ndivyo akuavyo
- Mganga hajitibu mwenyewe
- Mgonjwa haulizwi dawa
- Mcheka janga halijampata
- Kunguru mwoga hukimbiza bawale
- Debe tupu haliachi kuvuma
- Maji na hata yachemke vipi hayasahau kwao baridi
- Mtka cha uvunguni shariti ainame
- Ivute ngozi ingli bichi
- Samaki mmoja ameoza wote wameoza
- Dalili ya mvua ni mawingo
- Mwanamke mzuri hakosi kilema
- Mwenye macho haambiwi tazama
- Zimwi likujualo halikuli likakuisha
- Mwendakwao haogopi giza
- Ndege mjanja hulala juu ya mgude

- Ndege mwenye maneno mengi hana nyumba
- Ndovu hashindwi na pembe zake
- Ng′ombe wa kwanza hanywi maji machafu
- Njiwa huweza kuzaa mwewe
- Nyama ya nundu huliwa na mfugaji
- Palipo na mbuzi hapakosi wanambuzi
- Palipo na kwale hapakosi mwingine
- Penye vipofu wengi kengeza hufaidi
- Simba mwenda kimya ndiye mla nyama
- Ujirani mwema hutengeneza njia
- Ukimfukuza sana mjusi hugeuka nyoka
- Umande unaweza kuklunjiwa nguo lakini mvua haiwezekani
- Ukubwa si mali
- Watu hukataza tonge lakini sio mdomo
- Wema huzaa wema
- Vita havina macho
- Utamu wa kidonda unamuua nzi
- Utajiri ni kama umande.
- Usitukane wakunga uzazi ungalipo
- Usivuke maji usiyoweza kuyaoga

## MAZOEZI :

**Fafanua methali zifuatazo :**

1. Haba na haba hujaza kibaba
2. Pole pole ndio mwendo

3. Aliyeshiba hamjui mwenye njaa
4. Ajaye hupokewa
5. Jungu kuu halikosi ukoko
6. Kunguru mwoga hukimbiza bawale
7. Asiyekujua hakuthamini
8. Jungu kuu halikosi ukoko
9. gogo halianguki mara mbili
10. Mchumia juani hulia kivulini

## 1.2.4. NAHAU.

### 1.2.4.1. Dhana ya nahau

Nahau ni msemo uliojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini ambayo huwa inasetiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno hayo hayo iliyo katika matumizi ya kawaida.

**Mifano** :

- Ana jicho la nje−asherati
- Yeye ni jamvi la wageni−mwasherati
- Yeye ni bao la mkahawani=kahaba.
- Juma ana mkono wa birika=yeye ni mcoyo/mroho/bahiri.
- Kukata mitaa=Kutembea mitaani.
- Kulala fofofo=Kulala sana na kusahau kwenda kazini.
- Kufyata mkia=Kuogopa.
- Kuaga dunia=Kufa.
- Kujifungua=Kupata mtoto, kuzaa.
- Tumbo moto=Kuwa katika hali ya wasiwasi.

- Chungu nzima=-ingi sana.
- Kuvimba=Kukasirika.
- Kujiona=Kulinga.
- Kuvaa miwani=kuwa mtungi=Kuiandika tarakimu naane=Kulewa pombe.
- Kumpaka mtu matope=Kuongea vibaya juu ya mtu.
- Kuona cha mtema kuni=Kujuta, kupata shida.
- Kutoka=Kutakata=Kuvaa vizuri.
- Kuvunja ungo=Kuwa mwanamwali, kigori.
- Kupata kitanda=kulazwa hospitalini.
- Siku nenda rudi=Siku nyingi.
- Kupata jiko=Kuoa.
- Kumtoa mtu kijasho=Kumbabaisha mtu.
- Mfuko umetoboka=Kutokuwa nafedha.
- Hiyo ni mboga=Jambo rahisi.
- Kuponda raha=Kufurahi.
- Kwenda kujisaidia=Kwenda uani=Kwenda choo.
- Kwenda haja ndogo=Kwenda kukojoa.
- Kwenda haja kubwa=Kwenda kunya.
- Kaa chonjo=Tafadhari.
- Kuwa pete na kidole=Kuwa marafiki sana.
- Mbabe=Shupavu.
- Mzito=Mtu mwenye mali au madaraka.
- Kufunga majani=Kuwa na noti nyingi.

- Lugha chafu=Lugha mbaya.
- Kuwa mja mzito=Kuwa na mimba.
- Kutia chumvi=Kuongeza maneno zaidi ya yaliyokuwepo kwa kuchonganisha.
- Avya muye=Toa hasira au ghadhabu.
- Mbuzi=mtu ovyo
- Akina yaye=Mtu duni
- Kuchungulia kabuli=Kuwa mgonjwa mahututi, karibu kufa.
- Kufa kupona=Kwa kila hali.
- Kumezea mate=Kutamani kitu sana.
- Pua na mdomo=Kuwa karibu sana.
- Kupekua=Kutembea bila kuvaa viatu.
- Kuvimba=Kukasirika.
- Kula njama=Kufanya mpango wa siri wa kumfanyia mtu mabaya.
- Kupiga ubwana=Kukaa bila kufanya kazi wakati wa kazi.
- Kumwaga unga=Kupigwa kalamu=Kufukuzwa kazini.
- Kupana mwili=Kunenepa.
- Kwenda mwayo=Kupiga mwayo.
- Kwenda kombo=Kuwa nje ya mstari, mambo kuwa katika hali isiyo nzuli.
- Kwenda chafya=Kupiga chafya.
- Kuona cha mtemakuni=Kujuta, kuwa na shida ya jambo fulani.
- Mbavu za mbwa=Nyumba lilyojengwa kwa miti bila kukandikwa sawa.
- Kigingi=Taniboi.
- Kufunga mdomo=Kunyamaza.

- Hana masikio=Hatii
- Kuchongewa na ulimi=Kuponzwa na mambo yako mwenyewe.
- Kuvunja uso=Kuaibisha.
- Kupiga moyo konde=Kujipa moyo.
- Kupiga shabaha=Kulenga.
- Kupiga umalidadi=Kuvaa vizuri sana.
- Kutega sikio=Kusikiliza kwa makini.
- Kuyatia maneno sikioni=Kuyazingatia maneno.
- Kula miaka=Kufungwa kwa miaka mingi.
- Kujaa farafara=Kujaa tele, mpaka juu.
- Kwenda kapa=Kwenda kwa mikono mitupu.
- Kichwa tupu=Kutokuwa na akili.
- Kupiga swata=kutofanikiwa
- Kupiga domo=kuzungumza bila kufanya kazi
- Kushusha moyo=kukata tama
- Kushupaza moyo=kujipa nguvu
- Kula mwata =kupata taabu
- Kushuika taliki =kushika njia na klwenda
- Kuyoyoma=kwenda bila mpango
- Kakarakakara=hali ya kuwa katika mkukuriko, mshughulikohuku na huku
- Kukurukakara=tendo au hali ya kushughulika, kuhangaika, kubumburisha.

**MAZOEZI :**

Toa maana ya nahau hizi :

1. Kuvunja ungo

2. Kumezea mate
3. Kufa kupona
4. Kumpaka mtu matope
5. Kupiga soga
6. Kuwa mja mzito
7. kuvaa miwani
8. Kutia chumvi
9. Kuona cha mtemakuni
10. Kufyata mkia

## 1.2.5. NYIMBO

### 1.2.5.1.Dhana ya nyimbo

Wimbo ni utungo ulio na mdundo na mahadhi na unaoweza kuimbika. Nyimbo ni maarufu sana katika jamii nyingi za kiafrika. Nishughuli chache zinazoandamana na wimbo, densi au ngoma. Kuna nyimbo za : kazi, vita, tohara, harusi, kuzaliwa na kupatiwa jina kwa mtoto, kafara, matanga, kilio, na mazishi, sifa na nyimbo za mapenzi.

Nyimbo nyingi huelezea hisia za ndani za watu. Watu hucheza kwa nguvu zao zote kufuatia mdundo wa ngoma.

Sawa na hadithi na methali, nyimbo hufafanua hali ya jamii kisiasa, kijamii, na kiuchumi. Nyimbo huelezea pia historia, falsafa, imani na hekima ya jamii.

### 1.2.5.2. Aina za nyimbo

Kuna aina mbalimbali za nyimbo kufuatana na muktadha :

- Nyimbo za kubembeleza watoto/bembe/bembezi/bembelezi :

  Hutmiwa na wazazi au walezi kuwabembeleza watoto wachanga waache kulia au ili walale.

**Mfano :**

*Usiliye, usiliye*

*Ukaniliza Ingawa ziliimbwa na fanani mahususi zilizimamia maoni ya jamii kuhusu mape.nzi.*

*Nyimbo za matanga*

*Nyimbo za kisiasa*

*Nyimbo za tohara*

*Nyimbo za harusi*

*na mie*

*Machozi yako yaweke*

*Nikifa unililiye*

*Upigepike mateke watu wakuzuiliye.*

- Nyimbo za mapenzi : Nyimbo hizi ziliimbwa kuelezea hisia za mapenzi.
- **Nyimbo za matanga** : Hizi huimbwa wakati mtu anapokufa.Zinatofautiana toka jamii moja hadi nyingine, na hutegemea umuhimu na umri wa mtu aliyefariki.
- Jamii nyingi zinaamini kuwa kifo hakitokei tu, bali husababishwa na uovu wa mtu Fulani ama mapepo.Katika jamii zingine, kifo kinaonekana kama mwisho wa uhai. Inaaminika kuwa watu wanapokufa wanageuka na kuwa mizimu ambayo iko karibu sana na Mungu.

  Jamii nyingine zinaamini kuwa kifo ni faradhi.Hata hivyo bado utaona watu wakionyesha hofu kinapotokea.Kifo ni wakati wa huzuni na kuomboleza kwani kinamwondoa mtu mmoja miongoni mwa walio hai.

**Mfano :**

**KIFO :**

Hakuna sindano isiyokuwa na tundu

Hakuna wembe usiokuwa na makali

Kifo kinatujia kwa njia nyingi

Kwa miguu yetu tunatembea hapa duniani.

Kwa mikono yetu tunaigusa mbingu ya Mungu,

Siku moja hivi karibuni katika joto la adhuhuri,

Nitabebwa juu juu,

Kupitia kwenye kijiji cha wafu

Nikifa msinizike chini ya mti msituni,

Naiogopa miiba yake

Nizikeni chini ya kivuli cha miti iliyoko sokoni.

Nataka kusikia milio ya ngoma,

Nakuhisi ardhi itetemeshwa na wacheza ngoma.

- **Nyimbo za kisiasa** : Nyimbo zimetumika kikamilifu kama chombo cha kupinga ukosefu wa haki na kuwazindua watu ili wapiganie haki zao katika jamii.

  Nyimbo za kisiasa zaweza kugawanywa katika vitengo vitatu :

  - Nyimbo za kupinga uonevu katika jamii
  - Nyimbo za kuihamasisha jamii kisiasa
  - Nyimbo za kueneza kasumba au mawazo Fulani iliwatu wakubaliane na mkondo fulani wa kifikra.

- **Nyimbo za tohara** : Katika jamii zinazozingatia mila ya tohara, kuna nyimbo zinazoambatana na sherehe hii ndiyo maana katika jamii hizi kuna nyimbo mbalimbali za tohara.

- **Nyimbo za harusi** : Nyimbo za harusi ni zile zinazotumiwa katika harusi.Na arusi ni wakati wa furaha katika jamii nyingi.Lakini nyimbo zinazoimbwa huelezea masikitiko ya kuondoka mahali ulipozoea kwenda kusikojulikana.Nyimbo zingine humsifu Bi harusi na kumkejeli bwana harusi na familia yake.

**MAZOEZI :**

1. Andika wimbo wa kubembeleza mtoto kutoka katika jamii yako.
2. Toa wimbo mmoja wa mapenzi.
3. Nyimbo za matanga huwa zaimbwa wakati gani?
4. Tofauti gani iliyopo baina ya nyimbo za mapenzi na zile za arusi?

# SURA YA PILI : TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi ni aina ya matumizi ya lugha yanayohusishwa sana na ushairi hata wakati mwingine waandishi wa nathari.

Ni aina ya msemo fulani kwenye lugha unaojaribu kufupisha maelezo kwa kuchora picha ya aina Fulani wenye kujaribu kushawishi mawasijiano ya kisanaa kwa njia ya kufuma hisia kwa wasomaji au wasikilizaji.

1.**Tashbihi**.Hii ni mbinu ya uhusisho baina ya vitu viwili.Pia ni mbinu inayotumia uhamisho wa kimaana;yaani sifa, tabia, umbo, sura, muundo au umbo kutoka kitu kimoja huhamishwa kwenye kitu kingine, lakini hapa uhamisho au uhusisho si wa moja kwa moja, bali hupitia katika maneno kama : mithili, kama, mfano wa, vile, sawa, useme, na maneno mengine ya kuonyesha mlinganisho kati ya vitu mbali mbali.

**Mifano** :

a) Afya mwilini ni kama mafuta katika utambi wa taa

b) Ana upara kama jagwa la Sahara

c) Ali alinguluma useme simba mkali

d) Alikuwa na midomo mikubwa yenye nyama iliyojikunja kama pua ya nguruwe

e) Dunia ni kama uwanja wa mpira, kila mmoja anapasua kujua sehemu gani atapigania ushindi maishani mwake

f) Alikuwa na nyusi mfano wa mwezi mwandamano.

Katika sentensi ya, afya inalinganishwa na utambi wa taa.upara wa mtu fulani unalinganishwa na jangwa la sahara katika sentensi ya 2, katika sentensi ya tatu tunaona mgurumo wa Ali ulilinganishwa na ule wa simba n.k uhusisho huo ambao si wa moja kwa moja unjaotumia maneno kama : kama, mfano wa, useme….kuonyesha mlinganisho kwa vitu mbali mbali ni Tashbihi.

2.**Sitiari :** Ni tamathali ya usemi ambayo kwayo kitu matendo ya kitu au vitu kvyenye hulka mbali mbali, hulinganishwa na hali sawasawa ya maumkbile au jinsi ya utendaji.

Katika sitiari, maneno ya mlinganisho hayatumiki.Mlinganisho wa sitiari huifichwa ndani kwa ndani na hufichuliowa kwa his tu.

**Mifano :** 1. Kamau alikua simba

2. Mapenzi ni majani huota popote
3. Kukopa harusi, kulipa matanga
4. Tabia njema ni mzizi mkuu wa fadhila
5. Ujana ni moshi, ukenda haurudi tena
6. Maisha ya duniza ni bahari

**3.Tashihisi**Ni thamathali ya usemi ambamo kuna hali ya mlinganisho baina ya vitu viwili lakini sasa kimoja cha vitu hivyo ni chenye uhai na cha pili si kitu chenye uhai. Hiki kitiu kisicho na uhai au kisicho na tabia za kibinadamu hupewa sifa, tabia, sura au matendo ya kiuhai, au kiutu na kibinadamu.

**Mifano :** 1. Ubaya hatimaye utamezfwa na wema na sisi sote tushuhudie.

2. Wakati ulikua ukipiga mbio huwahi mwisho wa mtu yule.

Katika mfano wa 1, tumeona kwambaq wema unapewa uwezo wa kumeza kama vile mwanadammu anavyomeza kitu.Na katika mfano wa 2 tunaona wakati unapoewa uwezo wa kwenda mbio kama kitu chenye uhai.

*3.uhaba una ndwele mbi, una ndele mbi uhaba*

*Uhaba huleta dhambi, mtu hutamani kuiba*

Uhaba hupiga kambi, lango hutia bawaba

Katika ubeti huu kutoka shairi la Mathas E.Mnyampala tunaona kwamba uhaba unapewa uwezo wa kukumbwa na maradhi(ndwele), uwezo wa kumletea dhambi na uwezo wa kupiga kambi .

3.**TAASHIRA** : Ni namna ya fani ya usemi, ambao kwao, kwa sababu ya mwambatano wa ujamii au uhusiano mkubwa uliopo kati ya vitu fulani, ishara, alama, dalili, au neno Fulani, hutumika kuwakilisha tendo au kitu tupendacho kutaja, badala ya kueleza wazi wazi .

**Mifano :** 1. Shoka la kata miti msituni

2. *Anavaa kanzu za china*

3. kila nyumba ina furaha kubwa ya mazao

4. Fadhila nyingi na shangwe zilifika siteshoni ya treni mjini Dar es Salamu

Shoka lakata miti yametumika kawakilisha watu wenye kukata miti

Kanzu za china huwakilisha ka knzu zilizotengenjezwa uchina

Furaha majumbani huawakilisha watu wenye furaha nyumani, n.k

(i)Alama au ishara hutumika kufidisha hali fulani ya utendaji .(ii)kitu au chombo cha utendaji huwakilisha mtendaji au watendaji (iii)

Tendo huakilisha mtendaji.(iv)mahali kitu kilipotengenezwa huakilisuha kitu kitengenezwacho.(v)mtendaji huakilisha tendo.

**4.<u>Takriri</u> :** Ni kmtindo wa uneni wa fasaha, ambao msemaji kwa makusudi au nia mahsusi, hurudia neno au maneno yale yale ili kutia mkazo au msisitizo zaidi, juu ya jambo asemalo .Mtindo huu wa msemo wa msistitizo, huwa na nia ya kutia nanga jambo Fulani ili liweze kumwingia msikilizaji moyoni apate kulidhibiti vizuri.

Mifano : 1.Kifo hakiogopi kiumbe chochote duniani.Kifo hakimuopi mtawala au raia, Kifo hakina tajiri au maskini, kifo hakichagui mzee au chipukizi .Kifo hakina mkubwa au mdogo .Kila kitu chini ya mazingira kiomesha pigwa muhuri na kifo

2.Tulipo karibia kupambazuka, tuliusikia vurumai kubwa, ”

Mwizi.mwizi, mwizi huyo .Mkamateni mkamateni, mkamateni.Mwizi huyo mkamateni.”

**5.Tanakuzi :** Ni mtindo wa uneni wa fasaha ambao kwao maono au mawazo mbali mbali yenye mgongano na uhitilafiano, huunganishwa pamoja kakika sentensi au kifungu cha maneno ili kufanya mvutano mkubwa zaidi wa mawazo.

**Mifano :** 1. Kukonda rahisi kunenepa kugumu

2. Matengano ni huzuni makumbano ni lfuraha.

3. Baada ya dhiki, faraja

4. Hawa wanaingia hawa wanatoka

6.**Tabaini :** Ni mmtindo wa uneni wa fasaha, ambao kwao msemaji husisitiza kauli au ukweli na jambo Fulani kwa kutumia maneno yenye ukinzani, aghalabu neno “si”.

**Mifano :** 1. Lo, ama kweli Juma anafanana sana na babake, si kuwa, si nywele, si mdomo, si macho, si kichwa, si sauti !Ama baba na mwanawe wako kama pande mbili za sarafu.

2. Kwake watu wote walikuwa sawa, si mdogo, si mkubwa, si masikini, si tajiri.

Kwa kutumia neno “si”siyo kwamba twakanusha au kubomoa kauli tusemayo.

7.**Kinaya :**

Tamathali hii hutumika kwa kusemea kitu kimoja kwa kumaanisha kingine.Tamathali hii huweza kuonekana katika neno au kauli Fulani katika muktadha Fulani ilimojitokeza, au katika shairi zima.Kwa mmfano, shairi “Bustani”ya S.A.Muhammad, katika mojawapo wa beti zake, latongoa hivi :

*Yamerudikwa machicha, na maganda ya matunda.*

*Na mwiku uliochacha, na mbali uliovunda.*

*Harufu inopekecha, yanukia naipenda*

*Hakuna inomchusha, bustani ya maua.*

Kinaya hapa inajengwa kuanzia mustari wa tatu pale ambapo harufu inayopekecha kuwa inasemwa inanukia na kupendwa na hatimaye bustani na taka, machicha, maganda ya matunda ambayo unaambiwa hapana inomchusha.Kinyume kipo pia pale ambapo uchafu wa kupindukia huitwa bustani.

**8.Kejeli** : Hii ni tamathali inayofanyia stihizai, kebehi au dharau.Anayefanyiwa kejeli huwa anasutwa kwa kutupiwa maneno ya kero.

**Kwa mfano :**

Wanyakyusa wanaoishi Tanzania Kusini wanawakejeli Wazungu jinsi wapendavyo pesa kwa kutumia dini :

*Basikalija anasali wapi?*

*Kwenye mawe kwenye mawe*

*Watemi wanasali wapi?*

*Kwenye mizimu kwenye mizimu*

*Wazungu jee wanasali wapi?*

*Kwenye pesa kwenye pesa.*

9.**Tafsida** : Msemo wa adabu, ambao kwao mambo yasiyopendeza hatamkwi waziwazi, hasa hadharani, hutajwa kwa lugha ya siri bila kuchukiza au kuchafua moyo ili kinyaa au hali m, baya waonayo watu moyoni.

**Mifano :** 1. Acha naye aone cha mtemakuni, Mungu amemnyoshea kidole.

2. Mbona mtoto yule ana mkono mrefu vile!

3. Tafadhali nikumbushe, umenitoka machoni kidogo.

10.**Dhihaka** : Ni tamathali ya usemi ambayo inatumiwa kwa kusema maneno ya kumjukumu na kumdhihaki mwingine kisirisiri.

Mfano :

Bwana Bwanyenye wewe ni miongoni mwa matajiri nchini Tanzania, ama labda nikuite kabaila, nanyi makabaila wa siku hizi mu wakarimu sana.Juzi umetoa shilingi mooja kama ya dawa ikiwa ni mchango wako kusaidia ujenzi wa makao makuu ya TANU.

Ingawa maneno yaliyoambiwa bwana Bwanyenye juu ya kutoa shilingi ikiwa ni mchango wa kusaidia ujenzi wa makao makuu ya TANU ni ya sukari, lakini yalikuwa machungu moyoni.Msemaji hakuwa na nia ya kumsifu bwana Bwanyenye kama mtu mkarimu, bali nia yake ilikuwa kumdhihaki bwana Bwanyenye kama mtu bahili asiye na moyo wa uzalendo bora.

11.**Chuku** : Hii ina maana ya kutia chumvi jambo fulani linapojadiliwa.Kwa mfano, mwimbaji wa taarabu anapomwimbia mpenzi wake kuwa pendo lake lina thamani ya kuti ambayo usiku na mchana linang'aa na kuenea chumba kizima-hii ni chumvi tosha.

Pendo nlako nil la kutii moyoni limeshakaa

Mchana na lailati, nuru yake huzagaa

Ah! Mpenzi nimo peponi.

12.**Tanakali sauti** : Huu ni usemi unaoonyesha jinsi maneno ya lugha yanavyoweza kuiga sauti halisi.Kwa mfano, fisi anapotandikwa mwangwi wa mjeledi anasikika "chwaaa!"

Rangi yake ni nyeupe, ila si nyeupe pepe

Alikuwa na mweupe, wenye wekundu haiba

Njiwa huyu hulia kooo!!

## MAZOEZI :

Katika maandishi haya onyesha tamatali za usemi zilizotumiwa?

**1. Pendo**

Pendo, pendo wee!

Mbona huchoki kunisumbua?

Daima waninyanyasa,

Pendo adui ya wanadamu.

2.**Mpenzi Tanzania**

Tanzania, Tanzania!

Nakupenda kwa moyo wote,

Nchi yangu Tanzania,

Jina lako ni tamu sana!

Nilalapo nakuota wewe,

Niamkapo ni heri mama we!

Tanzania, Tanzania!

Nakupenda, kwa moyo wote!

3. suu ulimwengu **bahali tesi**
4. Kamau alikua **simba mkali**
5. mtoto huyo ana macho **kama ya kobe**
6. Nakwenda kwa **haja kubwa**
7. **Ndege walijaa uwanja wote hata sindano haionekani.**

# SURA YA TATU : MATUMIZI YA LUGHA

## 3.1. Rejista

### 3.1.1Dhana ya rejista

Rejista ni mtindo wa lugha inayotumika mahali penye shughuli mbalimbali na mazingira maalum.Kuna rejista za

mpirani, ofisini, hotelini, kisiasa, dini, uashi, uvuvi, upishi, na kadhalika.

### 3.1.2.Rejista mbalimbali

#### 3.1.2.1.Rejista ya dini

Picha inayoonyesha watu wanaosali



Dini ni taasisi muhimu katika maisha.Waamini na viongozi wao huelewana katika lugha yao.Hapa tutachukua mifano ya dini, kama vile dini ya kikristo na ile ya Kiislamu.Ipo lugha ambayo ukiisikia tu, utajua kuwa ni ya dini ya kikristo.

**Mfano :**

*"Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.Amina."*

Kwa kweli, dini ya Ukristo ndiyo tu yenye mafunzo ya ***"Utatu Mtakatifu".***Au basi, ukisikia watu wakisema maneno haya : "***Baba yetu uliye mbingunijina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni, utupe leo riziki yetu, utusamehe makosa yetu kama sisi tunavyowasamehe wanaotukosea. Usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu, kwani wako ni ufalme na nguvu hata milele.Amina***."Utajua wazi kuwa ni lugha ya dini ya kikristo.

Dini ya Kiislamu nayo ina lugha ya kuendesha mambo yake ya imani. Mwezi

Mfano : " ***Mwezi wa Ramadhani ni mwezi mtukufu watoba".***Usikiapo, utajua kuwa hiyo ni hotuba ya dini tena ni dini ya Kiislam.

***"Swalaa !Swalaa !".***Wito huo, mara moja mtu atajua ni wito wa sala au ibada na ni kwa ajili ya Waislam.

Ili mradi kuna lugha ambayo hutumika katika shughuli za dini.Katika hali ya mshangao na mshtuko, usikiapo mtu anasema ***"Mtume!"***au***"Yarabi",*** utajua ni mshangao wa mwamini wa dini ya KIislam.

### 3.1.2.2.Rejista ya kortini

Picha inayoonyesha mshitaki, mshitakiwa, majuji, na ***hadhira.***


Mahakama nayo pia huitumia lugha kwa namna yake.Ona mfano ufuatao.

***Askari :*** Kooriti!

(Watu wanasimama, hakimu anaingia.Hakimu anakaa na watu wote wanakaa).

***Karani*** : Kesi namba 23/41/10

Mshitakiwa ni***MASEZERANO MAWIKE JeanWycliffe***



Mshitaki ni***MPAYIMANA Cyprien***

Mshitakiwa anashitakiwa kwa kosa la kumpokonya hela mshitaki tarehe 31 Mei 2012 saa mili usiku katika ***Tella Vista Hôtel***.

***Hakimu*** : Je, unakubali hatia?

***Mshitakiwa*** : Sina hatia.

***Hakimu*** : Wewe dini gani?

***Mshitakiwa*** : Mwislam!

***Hakimu :*** Shika Korani na apa!

Sema baada yangu :

Naapa!

Wallah!

Wabilahi!

Nitasema kweli.

Kweli tupu!

Na Mungu anisaidie!

Lugha kama hiyo ni vigumu kuipata popote ila mahakamani, au katika mchezo wa kuigiza unapoonyesha mambo ya mahakama.

### 3.1.2.3.REJISTA YA OFISINI

Ofisi nazo zina rejista zake.

Mfano :

***Mgeni*** : Hodi!

***Katibu*** : Karibu!

Karibu kiti.

***Mgeni*** : Ahsante.

***Katibu*** : Sijui nikusaidie nini!

***Mgeni*** : Nahitaji kuonana na Mkurugenzi kama yupo.

***Katibu*** : Shida ya binafsi au ya kazi?

***Mgeni*** : Ya binafsi.

***Katibu :*** Mnafahamiana?

***Mgeni*** : Hapana! Ila ni tatizo la binafsi.

***Katibu*** : Hata jambo la kazi mara nyingi humhusumtu binafsi japo si jambo la kibinafsi.

***Mgeni*** : Hapana.Mimi nahitaji kazi tu!

***Katibu*** : Ulishaandika barua?

***Mgeni*** *:* Hapana.Samahani!

***Katibu*** *:* Bila Samahani!

Karibu tena.

Haya ni mazungumzo ya kikazi na mtindo wake ni tofauti kabisa na ile lugha ya mahakamani.

### 3.1.2.4. REJISTA ZA JAMAA

Kila rika ina aina ya utumiaji wake wa lugha.Rika hizi ni za aina tatu kuu yaani, watoto, vijana, watu wazima au wazee.

**a)** **Watu wa rika tofauti** (Mfano wa mtoto na babake)

Watu wasiolingana katika umri ni vigumu kabisa kuwa na lugha kama watuwanaolingana. Vijana wakizungumza wenyewe kwa wenyewe huwa na lugha yao.Watoto nao vilevile wakizungumza wenyewe kwa wenyewe huwa na lugha yao;an wazee hivyo hivyo.Lugha hizo huwa tofauti katika mazungumzo, pia katika lugha ya kuandika.Hebu tutazame lugha ya kijana ***Masezerano***, akizungumza na mzee wake au mzazi wake ***Mpayimana***.

***Masezerano*** : Shikamoo baba!

***Mpayimana*** : Oh! Marahaba***Masezerano***!

Umefika lini?

***Masezerano*** : Nimefika sasa hivi.

***Mpayimana*** : Kaa basi mbona una wasiwasi.

***Masezerano*** : Hata! Sina wasiwasi mzee.

***Mpayimana*** : Habari za shule!

***Masezerano*** : Nzuri sana! Hapa kuna barua kutoka kwa mkuu wa shule.

***Mpayimana*** : Matokeo ya mtihahani bila shaka!

Aa! Umefanya vizuri mwaka huu.Umekuwa mtu wa kwanza.Haya nenda kapumzike, mwanangu.

***Masezerano*** : Ahsante, baba!

Toka mwanzo utaona ni mazungumzo yanayoonyesha utamaduni wetu wa Kiafrika, kuwa kijana anamheshimu mzazi wake hata katika kuongea.Lugha hii hutumika si kwa mzazi tu bali lugha ya adabu hutumika kwa wote ambao ni wakubwa kwetu kwa umri na hata kwa cheo na madaraka.Katika utamaduni wa Kiafrika "kiburi si uungwana", adabu na adili ndiyomsimamo wetu.

**b) Mfano wa mtu na mkwewe**

***Mama mkwe*** : Mmeamkaje akina baba?

***Mkwe wa kiume*** : Tumeamka salama.

Shikamooni.

***Mama mkwe*** : Marahaba.Mnajisikiaje na uchovu wa safari?

***Mkwe wa kiume*** : Hatujambo kabisa.

Na nyie mmeamkaje?

***Mama mkwe*** : Tumeamka salama, tunashukuru.

***Mkwe wa kiume*** : Mama, leo naona tutasafiri.

***Mama mkwe*** : Ah! Mara hii!

***Mkwe wa kiume*** : Samahani mama tumekuja kwa shughuli ya haraka, hivyo lazima turudi kazini.

***Mama mkwe*** : Haya baba! Basi muwasalimie huko nyumbani.

***Mkwe wa kiume*** : Haya ahsanteni, make salama.

## 3.1.2.5.REJISTA YA HOTELINI

Picha inayoonyesha wateja wanaokula chakula hotelini



Hapa, wasafiri watatu wanalonga na mwenyeji wa hoteli :

***Msafiri wa kwanza*** : Chai moja hapa.

Silesi na macho ng'ombe mbili.

***Mwanye hoteli*** : Wewe?

***Msafiri wa pili*** : Mimi chai na silesi kavu

***Mwenye hoteli :*** Mmh?

***Msafiri wa tatu*** : Mchuzi juu na mtindi.

***Mwenye hoteli*** : Na wewe tena?

***Msafiri wa kwanza*** : Mimi strungi mbili na makongoro.

***Mwenye hoteli*** : (huku akileta vyakula).

Nani macho ng'ombe! Wapi?

***Msafiri wa kwanza*** : Mimi.Hapa!

***Mwenye hoteli*** : Nani mchuzi juu, nani strungi na makongoro?

Haya, chapuchapu!

### 3.1.2.6.REJISTA YA MPIRANI

Picha inayoonyesha wachezaji na mashabiki uwanjani

Kuna aina nyingi za michezo ya mpira, lakini mpira wa miguu umetia fora sana duniani;hapa Rwanda na Afrika nzima.Mchezo huo umepata majina mengi ambayo hutumiwa mpaka sasa, kama vile soka, kabumbu, kipute, gozi, kandanda, ruhago, na majina mengine mengi. Watazamaji au mashabiki wa mpira huwa na lugha maalum kuelezea matukio yanayotokea uwanjani.Watangazaji wa redio nao, kwa upande mwingine, wanapotangaza mpira huwa wanatumia rejista maalum.

Kwa mfano :

- ***Kuvisha kanzu*** : Kkpitisha mpira juu ya kichwa cha mchezaji.
- ***Kutoa bomba*** : Kuupiga mpira kwa nguvu.Pia, "kupiga mkwaju" au "shuti".
- ***Mpira kuwa mwingi*** : Mpira kutoka nje ya kiwanja.
- ***Kukokota ngoma*** : Kwenda na mpira.



- ***Kukata mbuga*** : Kukimbia na mpira au kwenda mbio na mpira.
- ***Mpira kuambaambaa nje*** : Mpira kwenda nje huku ukiwa sambambasambamba na mstari wa pembeni mwa kiwanja huku ukiwa unatambaa ukigusana na ardhi.

- ***Kuunawa mpira*** : Kuushika mpira kwa mikono, hali mchezaji huyo hastahili kucheza mpira kwa mikono.
- ***Kuotea :*** Ni kuzidi, yaani mchezaji kwenda sehemu asiyotakiwa, sehemu ya adui akiwa peke yake.
- ***Harusi*** : Mpira kupita katikati ya miguu ya mchezaji uwanjani.
- ***Kuunyaka mpira*** : Kuudaka mpira.Mara nyingi huwa ni mlinda-mlango (au golikipa) anayefanya hivyo.
- ***Refa/mpiga kipenga/mpiga filimbi*** : Mwamuzi mkuu wa mpira.
- ***Washika vibendera*** : Waamuzi wengine wawili katika soka.

## MAZOEZI

1. Bwana MASEZERZNO MAWIKE Jean Wycliffe anashtakiwa kwa kuendesha gari bila uangalifu wala kubonyeza kwa breki, siku ya Ijumaa tarehe 19/12/2012, saa nne unusu usiku na kugonga gari la bwana MPAYIMANA Cyprien taa nne zikavunjika, katika ajali iliyotokea siku hiyo saa hizo huko Kicukiro karibu ya Tella Vista Bar.

   Je, tukio hili laelezwa kwa kutumia rejista zipi?
2. Toa rejista tano zinazotumiwa katika kipute.
3. Je, ni rejista zipi unazozitumia sokoni wewe?

# SURA YA NNE : MNYAMBULIKO WA VITENZI

## 4.1.UNYAMBULISHAJI WA VITENZI

Unyambulishaji wa vitenzi ni utaratibu wa uundaji wa vitenzi vipya katika lugha kwa kuongeza viambishi nyambulishi kwenye maumbo ya mizizi. Katika lugha ya Kiswahili kuna viambishi nyambulishi ambavyo vinatumika katika uundaji wa vitenzi vipya kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo :

**Mifano :** a) pend+a

b) pend+e+a

c) pend+ele+a

d) pend+ele+an+a

e) pend+ez+a

f) pend+ez+esh+a

g) pend+ez+esh+an+a

Katika mifano hii, kutokana na mzizi wa kitenzi **pend-,** tunaweza kupata maneno kama yale yaliyoorodheshwa katika mifano ambapo viambishi tamati –e, -an, -ele-, -esh, ni nyambulishi kutokana na kufanya maumbo yanayohusika kuwa vitenzi vyenye maana tofauti.

Katika Kiswahili kuna viambishi nyambulishi vinane ambavyo huambikwa kwenye mizizi ya vitenzi ambavyo ni pamoja na : -w-, –ik-/-ek-, – ish/-iz-/-esh-/-ez-, –il-/-el- n.k

Viambishihivyo huonyeshahali ya vitenzi :

1. **Hali ya kutendua**.Ni hali inayonyesha kinyume cha kitenzi kinachotajwa **Mfano** : tendua, Anua, fungua, fukua, tatua
2. **Hali ya kutendewa** : Mtu alliyefanyiwa jaambo Fulani ndiye anayezungumza **mfano :** chumbiwa

pigiwa

adhibiwa

imbiwa

3. **Hali ya kutendwa** : Hapa mtu mtendwa ndiye huwa amefanyiwa jambo Fulani

   **Mfano :** pigwa

   liwa

   chorwa

   vunjwa

   katwa

4. **Hali ya kutendeka** : Hapa vitenzi hueleza kuwepo kwa uwezo wa kitendo cha kitenzi kutokea

   **mfano** : someka

   imbika

   ombeka

   fungika

5. **Hali ya kutendeana** : Katika hali hii ya kunyambuwa mtu anamtendea mwingine jambo, naye huyu aliyefanyiwa anamfanyia mwenzake kitendo hicho hicho **Mfano :** katiana

   vunjiana

   simamiana

   tendeana

5. **Hali ya kutendesha** : Nayo sh, z, au vy katika mnyambuliko huleta maana ya kusababisha. Kwa hiyo vitenzi vyote katika hali hii huonyesha kuwa vimesababishwa na hali, kitu ama mtu Fulani.

## VIAMBISHI VYA NAFSI

Vitenzi huwa na viambishi vya nafsi ambavyo ni pamoja na ni-, u-, a -, tu -, mu-, wa-, ku-, n.k

**Mifano :**

ni : **Ni**merudi nyumbani,

u : **U**takuja kesho,

a : **a**nalala salama,

**tu :** tumerudi

m : mmekuja

wa : wamekuja

Katika mifano hii viambishi vinawakilisha nafsi katika nafsi ya kiima.

Ni : ni nafsi ya kwanza umoja

U : nafsi ya pili umoja

A : nafsi ya tatu umoja

Tu : nafsi ya kwanza wingi

M : nafsi ya pili wingi

Wa : nafsi ya tatu wingi

### Viambishi vya njeo

Viambishi vya njeo hujitokeza katika maumbo ya vitenzi kuonyesha njeo ya vitenzi. Viambishi hivyo ni pamoja na : -li-, -me-, -na-, -ta-, -ku-, -ja-, -hu-, -i.

**Mifano** : a) wakati uliopita(kukubali)

Ni-**li**-kula

Wa-**li**-tutafuta

b) wakati uliopita hali timilifu(kukubali)

tu-**me-**soma vizuri

wa-**me**-tembea kwa miguu

c) wakati uliopo(kukubali)

u-**na**-sema Kinyarwanda

ya-**na**-liwa

d) wakati ujao(kukubali)

vi-**ta-**semwa

wa-**ta-**enda

e) wakati uliopita(kukanusha)

ha-**ku**-nichosha

f) wakati uliopita hali timilifu(kukanusha)

ha-ja-enda

ha-ja-wa-ona

g) hali ya mazoea(kukubali)

kila siku **hu-**tu-tembelea

watoto**hu**-fundishwa

### viambishi vya hali

viambishi vya hali ni viambishi ambavyo huonyesha dhamira ya maelezo. Viambishi hivyo ni pamoja na : -a-, -e-, -o-, -ka-, -ki-, -li-, -nge-, -po-, -ngali-, –ngeli-.

**Mifano :** ali**po**niona aliniambia habari zake

Wa**ngali**mtafuta wa**ngali**uliza baba yake

### Viambishi virejeshi

Ni viambishi vinavyowakilisha kitajwa katika umbo la vitenzi .viambishi hivyo ni : o, lo, cho, yo, vyo, zo.

**Mifano :** wali-**o-**kuja wamepata zawadi zao

Una-**vyo**-sema vinaniumiza

### MAZOEZI :

1) Onyesha viambishi vya nafasi, vya njeo katika vitenzi vifuatavyo :

Utakuja kesho

Tutaonana

Ninakupenda sana

Tutafika kesho

Akirudi nitamuona

2) Unda vitenzi kutoka vitenzi vifuatavyo :

Piga

Chafua

Pika

Lewa

# SURA YA TANO : UHAKIKI

## 5.1. DHANA YA UHAKIKI (MAANA)

Uhakiki huchukuliwa kama utathmini, ufasili na uainishi wa kazi za fasihi. Haimaanishi kuitafutia makosa kazi hiyo. Uhakiki kama kitendo cha kiakademia humaanisha maoni ya msomaji kuhusu kinachotendeka kitabuni.

Hapo twaona kwamba uhakiki unahusu utathmini na tafsiri ya mambo yanayopatikana katika kazi anayoizingatia mhakiki. Lakini pia twaona maoni yao finyu yanayoiona kazi kama ya kiakademia na pia kuyihusisha na fasihi andishi.

Kwa machache uhakiki ni kazi ya kutathmini na kueleza, kuainisha na kutoa maoni kuhusu kazi mbalimbali za fasihi.

## 5.2.SABABU ZA UHAKIKI

1. Kuichambua kazi ya kifasihi au kuieleza kulingana na misingi yake kwa hadhira.
2. Kuichambua kazi ya fasihi ili kujua misingi ya ubunifu wake na kutambua thamani yake.
3. Kuelezea sheria kwa waandishi na kuifafanua juu ya uzuri kwa hadhira.
4. Kuifafanua kazi isiyoeleweka kwa wasomaji ili wapate kuielewa vema.
5. Kuzihukumu kazi za kifasihi kwa kuzingatia misingi maalum ya uhakiki iliyokwisha wekwa.
6. Kugundua na kutumia misingi ambayo huieleza misingi ya kazi nzuri ya kifasihi.

## 5.3. AINA ZA UHAKIKI

A. **Aina ya kivionjo au kihisi :** aina hii huachambua na kuyahakiki maandishi ya kifasihi kama yanavyomwathiri mhakiki. Mhakiki huyasifu au kuyakosoa maandishi kufuatana na vile yanavyomgusa.

Kwa kuzingatia aina hii mhakiki anapitia mambo yote ya msingi katiki kazi ya kifasihi. Mhakiki ataangalia matumizi ya lugha, ujenzi wa wahusika, mtindo na muundo, mandhari, na hatimaye atachambua vipengele vinsvyohusu maudhui. Anaweza pia na uhakiki wa maudhui.

Aina hii inaweza kuwa na athari tofauti sana kati ya mwandishi na mhakiki, na kati ya mhakiki na wahakiki wengine watakaokuwa wamepitia kazi hiyo.

B. **aina ya kihistoria au kisosiolojia :** wakati mwingine, mhakiki huamua kuikabili kazi ya fasihi kwa kuangalia jinsi kazi hiyo inavyohusiana na mazingira ya kihistoria yanayomuhusu mwandishi na maisha yake.

Maandishi huangaliwa kufuatana na wakati wake wa kuandikwa, habari inayozungumziwa, hali za wahusika, mandhari, vifaa na maisha ya mwandishi mwenyewe.

Aina hii kimsingi hutawaliwa na imani kuwa uhusiano kati ya kazi ya kifasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu sana. Uchunguzi wa mahusiano wa mambo ya kijamii unawza kusaidia kuona uzuri wa kisanaa wa kazi ya kifasihi.

Sanaa haijengwi katika ombwe. Ni kazi ya mwandishi katika mazingira na wakati mmalum akiwajibika kwa jamii inayomhusu ambayo ni sehemu yake muhimu.

Mhakiki wa kihishoria, ambaye wakati mwingine hujulikana kama mhakiki wa kisosiolojia analazimika kuelewa mazingira ya kijamii na jinsi yanavyoathiri kazi anayohakiki.

C. **Aina ya kiufafanuzi :** Aina nyingine ni ile ya ufafanuzi wa maandishi kama maandishi. Aina hii huiangalia kazi ya sanaa kama kitu kisichohusiana na jambo jingine lolote nje ya kazi yenyewe.

"ushairi hauhusiani na jambo lolote nje ya kazi yenyewe. Ushairi hutegemea jinsi vipengele vyake mbalimbali vinavyohusiana : muundo n.k." kwa mtazamo huo, mhakiki huikabili kazi ya kifasihi kwa kuchunguza vipengele vya kazi hiyo na kuona jinsi vinavyohusiana na kuangalia maana ya shairi inavyopatikana kutokana na vipengele hivyo : mizani, taswira, uteuzi wa maneno, ubeti, pamoja na umbo sauti (toni), dhamira, n.k ambavyo hufanya kazi pamoja na si katika utengano, katika kuleta maana ya shairi. (kazi ya kisanaa)

Katika aina hii, mhakiki huchungua msimamo wa mwandishi, huchungua maandishi kwa kuyatafsiri ili kugundua maana iliyomo, hutoa uhakiki wa mambo ulivyo, kulinganisha maandishi hayo na maandishi mengine, na hatimaye mhakiki hujenga msimamo wake kuhusu maandishi yanayohakikiwa.

**D. Aina ya kimaadili :** aina ya kimaadili huiangalia kazi kufuatana na maisha ya watu. Aina hii, ina historia ndefu kuliko nadharia nyingine za kihakiki. Kwa mfano PLATO alihushika sana na athari za maadili ya mshairi katika kitabu chake cha *the republic*.

Nadharia hii inadai kuwa umuhimu wa fasihi hautokani tu na jinsi ya kusema, bali pia katika kile kinachosemwa. Mara nyingi hii huelezwa katika mtazamo wa "fani na maudhui", tofauti na aina ya kiufafanuzi ambayo husisitaza ama kujali jinsi ya kusema jambo. Nadharia ya kimaadili hujali yote : jinsi ya kusema na nini kinachosemwa. Wahakiki wanaotetea mtazamo huu huingalia fasihi kama kitu kinachohakiki maisha ya mwanadamu. Kwa wahakiki hao, mbinu za kujifunza fasihi ziwe njia za kufikia welewa wake kama kitu kinachoathiri maisha ya mtu. Mtu anaangaliwa kama kiumbe aliyetofauti na wanyama kutokana na uwezo wake wa kiakili na misingi ya kiutu aliyo nayo.

**E. Aina ya kisikolojia :** aina hii huanza na dhana kuwa mtu ametekwa nyara na mazingira anayoyaishi. Kwa msingi huo mtu hayuko, na wala hatakuwa huru hata kama angependa awe huru.

Kwa upande mwingine, mhakiki wa aina hii hulazimika kuyafahamu maisha ya mwandishi wa kazi ile anayoihakiki.

Hii itamsaidia mhakiki kuelewa kwa kiwango ambavyo maisha ya mwandishi yanayojitokeza katika kazi ya kifasihi. Saikolojia ya mhakiki, kama elimu muhimu aliyo nayo, humsaidia mhakiki kudadisi na kubuni kile ambacho huenda mwandishi alitaka kukisema. Zaidi ya hayo mtazamo huu unadai kwamba kuna uhusiano wa huduma na ulio muhimu kati ya mwandishi na kazi yake. Wakati mwingine mwandishi ametazamwa kamamgonjwa ambaye hutibu maradhi mwenyewe kwa kuyaandikia vitabu. Mhakiki hatimaye atafanya uchambuzi wa kazi hizo zilizoandikwa na "mwandishi mgonjwa" kwa kuipima kazi hiyo na kuifasili juu ya yale ambayo mwandishi ameyasema. Mhakiki atayagundua mambo yasiyojulikana ambayo huenda mwandishi alikuwa nayo. Aina hii inasidia mambo humihu kadhaa : kwanza, matatizo

binafsi ya wandishi hujulikana kwa kiasi kikubwa. Pili, mikondo ya waandishi mbalimbali inaweza kugundulika na kufahamika kwa wasomaji na wahakiki. Tatu, saikolojia inaweza kutumika katika kuelezea wahusika na matendo yao ambayo yanaonyesha uhalisia fulani ya maisha ya watu.

F. **Aina ya kitanzu :** aina hii huhakiki kazi ya kifasihi kwa kuzingatia misingi ya utanzu wa kifasihi unaohakikiwa. Mhakiki anayeamua kufuata aina hii anajitahidi kuangalia sifa za kila utanzu. Kimsingi, tanzu zote za kifasihi zinahusiana kwa njia moja au nyingine. Lakini kwa upande mwingine, pamoja na kufanana huko, kuna muhimu zinazopambanua utanzu unaohusika.

Kwa msingi huo tunaweza kuuchambua ushairi kwa kuzingatia misingi ile inayoujenga na tamthilia nayo tukachambua kwa misingi yake, hata hivyo ni muhimu kusisitiza kuwa kuna uwezekano wa kuingiliana katika misingi na mikabala kwa masuala yanayohakikiwa na wahakiki.

## 5.4. UMUHIMI WA UHAKIKI

- Baada ya kufanya uhakiki wa kazi ya fasihi Fulani mahali ambapo kuna migogoro, humfanya mhakiki kuwa muumbaji wa sanaa na kujipambanua mwenyewe na kujiweka katika tabaka Fulani.
- Kwa kufanya uhakiki, mhakiki anaweza kuielewa histolia ta watu ambao maandishi hayo yanawahusu.
- Uhakiki husaidia wasomaji kuelewa mazingira wanamoishi na kupambana nayo.
- Uhakiki husaidia kueleza mambo kiwaziwazi ili kupata suluhisho.
- Hatimaye, mhakiki hujikuta ana kazi ya kumfundisha msomaji juu ya yale yaliyomo katika kazi ya sanaa na kumfundisha mwandishi juu ya yale aliyoyasema yanavyoweza kupokelewa na jamii.
- Uhakiki inatetea silika na matakwa ya umma.

## 5.5 JINSI YA KUFANYA UHAKIKI

Kazi ya uhakiki inafanywa kwa kuzingatia vipengele muhimu katika uchambuzi wa kazi mbalimbali za fasihi. Vipengele muhimu ni hivi vifuatavyo :

### 1. WAHUSIKA

Wahusika ni watu, wanyama au vitu katika kazi ya sanaa ya kifasihi. Mhakiki analazimika kuuelewa uhusika wa kila mhusika katika kazi ya fasihi inayohakikiwa. Wahusika wanagawika katika aina kuu tatu.

- **Wahusika wakuu**

  Mhakiki anatakiwa kuwatambua wahusika wa aina hii wakati wa uhakiki wake. Hawa ni wale ambao wanajitokeza kila mara katika kazi za fasihi tangu mwanzoni hadi mwishoni.

- **Wahusika wajenzi**

  Wahusika wa aina hii, sanasana wanapatikana kwa kumsaidia mhusika mkuu katika vitendo vyake.

- **Wahusika wadogo**

  Kimsingi, wahusika hawa sio muhimu sana kama wahusika wakuu. Wao hujitokeza hapa na pale katika kazi ya fasihi wakiwa na lengo la kuukamilisha ulimwengu wa kazi zao.

  Wahusika wadogo pia huisaidia kuijenga dhamira kuu, au dhamira Fulani inayojadiliwa katika kazi ya fasihi. Aidha, kwa vile kazi yao ni ndogo hata kama wakikosekana hawawezi kuiathiri sana kazi ya fasihi.

### 2. MTINDO

Mtindo unaweza kuelezwa kwa maana mbili : kwanza, ni ile maana mwandhishi ameitumia katika kujenga kazi yake. Ni namna ile ambayo yeye kama msanii huipa sura ambayo kifani na kimaudhui itakuwa tofauti na nyingine iliyoandikwa na mtu mwingine.

Wakati mwingine kile kinachoelezwa huitwa pia mtindo. Kwa kutumia dhana hiyo, tuna mtindo wa upelelezi, mtindo wa mapenzi, mtindo wa dini, mtindo wa siasa, mtindo wa kishairi, mtindo wa tamthilia na kadhalika.

Kwa machache **mtindo** ni upangaji wa **fani** na **maudhui** katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hatimaye hutokeza au huonyesha nafsi na labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo.

**3. MUUNDO**

Muundo ni mfululizo au mtiririko wa matukio yanayosimuliwa katika hadithi. Mhakiki anapofanya kazi yake anajalibu kuchunguza jinsi mwandishi alivyounda au kufunua na kuunganisha matikio yake, vitendo, mawazo, na kadhalika.

Badhi ya kazi za fasihi zina muundo wa moja kwa moja, unajumuisha maelezo rahisi kwa kukua hadi mwisho.

**4. LUGHA**

Lugha ndicho kipengele muhimu katika kazi yotyote ya sanaa ya kifasihi. Matumizi ya lugha ndiyo yanayofanbya kazi Fulani ionekane tofauti na nyingine awa itofautishe kazi ya sanaa ya kifasihi na isiyo ya kifasihi. Lugha ndiyo mzizi wa kazi ya fasihi, kwani fasihi ni kazi ya sanaa inayotoa maudhui yake kwa kutumia lugha ya maneno.

Matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi yako ya aina mbalimbali : nahau, misemo, methali, tamathali za semi, lugha za lahaja, miundo ya sentensi, uteuzi wa maneno na kadhalika.

## 5.6. SIFA ZA UHAKIKI

- Uhakiki ni kazi bora inayofanywa na mhakiki ambaye ni mzoefu wa kazihiyo.
- Uhakiki ni kazi ambayo inalenga mazingira ya msomaji
- Uhakiki unafinyanga ulimwengu kuhusiana na hadhira
- Uhakiki ni kazi inayolenga kazi mbalimbali za kifasihi
- Uhakuki hbadilisha maisha ya wasomaji ikiwa mhakiki ni imara

## 5.7. MATATIZO YA UHAKIKI

- Mhakiki anaweza kukumbwa na migogoro katika kazi yake ya kutathmini kazi Fulani ya kifasihi kama lugha ngumu ya msanii
- Uhakiki waweza kufanywa kwa njia ya kiholela au njia isiyohalali kwa sababu ya udhaifu wa mhakiki
- Hadhira yaweza kuwa ya watu si wasomi

## ZOEZI

UA LA MOYONI UA

Ua la langu la moyoni, ua nituze nipowe

Ua langu sinihini, ua nipoze nituwe

Ua nikae shingoni, ua usiniambuwe

Ua la moyoni ua, ua lichanuwe kwangu

Ua lichanuwe kwangu, kama koja lichanuwe

Ua sinitoke kwangu, ukawa na nwinginewe

Ua ewe uwe wangu, milele mimi na wewe

Ua la moyoni ua, ua lichanuwe kwangu

Ua nipe liha njema, riha njema ninukiwe

Ua nipoze mtima, ua nipoze nipowe

Ua nikae daima, daima mimi na wewe

Ua la moyoni ua, ua lichanuwe kwangu

Chambua shairi hili kwa kuonyesha :

- Muundo
- Mtindo

- Matumizi lugha
- Wahusika
- Mandhari/mazingira
- Na mbinu nyingine za kisanaa

# SURA YA SITA : UFUPISHO

## 6.1.Dhana

Neno “**ufupisho**” linatoka katika neno **fupisha**” maana yake ni kufanya kuwa fupi au kupunguza urefu. Na kwa hiyo, neno ufupisho linatumiwa kutoa muhtasari wa habari. Hii ina maana kwamba baada ya kusikiliza habari fulani kwa mfano hadithi fupi au baada ya kusoma kazi Fulani pengine unatakikana kufupisha kazi hiyo kwa maneno yako mwenyewe.

Ni muhimu sana kujifunza ustadi wa ufupisho kwa sababu mara nyingi katika maisha yako utawahi kukumbana na kazi za aina nyingi ambazo zitahitaji kuzifupisha. Kwa mfano, mara nyingi itakulazimu kufupisha kazi mbalimbali za fasihi kama hadithi fupi, riwaya, tamthilia, mashairi, n.k.

Kabla hujaendelea mbele zaidi, ni muhimu kuelewa kwamba ufupisho wa kazi yoyote ile unaweza kulinganishwa na maharagwe au mtama ambapo mazao hayo yote yamevunwa shambani. Kwa kawaida mazao hayo yatavunwa, yaanikwe na kukaushwa. Baadaye mazao hayo yaliyo na maganda yake yatapigwapigwa au kupondwapondwa ili kupata mbegu ambazo ndizo zinatakwa kwa chakula au kuuzia.

Sasa kumbuka kwamba ukitoa maharagwe au nafaka za mtama kutoka maganda yake, utapata mbegu kidogo kuliko maganda yatakayobaki na kutupwa shambani na kutumiwa kama mbolea. Na kwa hiyo kama tufanyavyo kupata mbegu kudogo kutoka rundo la mbegu zenye maganda na baadaye kutupa maganda tusiyoyataka, ndivyo tufanyavyo ili kuchambua kazi za muhimu fasihi kutoka katka hadithi fupi, mashairi marefu, riwaya, tamthila, n.k.

Kwa kielelezo hiki, ufupisho ni kuchambua habari iliyo muhimu katika rundo ya habari kutoka kazi fulani ya kifasihi iliyo na “maganda”.

## 6.2.Utaratibu wa kufuata ili kufupisha kazi za fasihi

1. Kwanza soma taarifa ya kazi ya fasihi uliyopewa kwa makini mara mbili au mara tatu mpaka upate kuelewa kiini cha kazi ya fasihi.

2. Andika mambo muhimu kwa muhtasari.
3. Panga vizuri muhtasari wako wa mambo muhimu ili kazi iwe na maana pamoja na ufungamano wa mawazo.
4. Sasa panua muhtasari wako kwa maelezo kataka sentensi kwa maneno yako mwenyewe.
5. Jaribu kutumia msamiati unaofaa. Badala ya kutumia maneno kadhaa kueleza jambo, inafaa kutumia neno moja lenye maana hiyohiyo.
6. Hesabu maneno ya ufupisha wako ukilinganisha nay ale ulioagizwa kutumia.
7. Sahihisha muswada wa ufupisho wako ukiondoa mambo, maneno, sentensi au vifungu vya maneno visivyofaa huku ukikadiria urefu wa ufupisho unaotakikana.
8. Sasa andika ufupisho wako wa kazi kwa nathari katika aya moja. Jalibu kuandika vizuri ili mwandiko wako usomwe kwa urahisi.
9. Andika idadi ya maneno uliyotumia kataka ufupisho wako mwishoni katika vifungu vya mibano.
10. Inaweza kuwa vigumu kutumia idadi kamili ya maneno yaliyopendekezwa. Kwa hiyo unaruhusiwa kuwa na upungufu au yaidi ya maneno kumi kwa yale yaliyopendekezwa.

### Mfano

**Hadithi fupi : *Sauti ya mauti***

Mzee Mauti aliishi katika kijiji cha Cheleamambo. Kwanza hatuna kati yetu hata mmoja anayeweza kufafanua ni kwa nini aliitwa jina hili Mauti. Hatuwezi kuhakikisha kama jina hili ni lake halisi au alipangiwa.

Mzee Mauti alizoea ukaliukali tu. Hakuna kitu alichokipenda kuliko vita na mapigano. Alikua mwanamieleka jabari sana. Hakuna mpinzani yoyote aliyewahi kumuangusha chini. Kwa ndondi alikuwa nyundo.Alikugonga ngumi moja, sharti urambe ardhi.Na ukifanya mzaha, huamki mpaka unyweshwe maji lita tatu.

Kati ya watu walioogopwa kitongojini pale Mauti. Hakuwa na rila aliyemkabili. Sauti yake pekee ilitisha na kuogofya kuliko mtu mwenyewe. Licha ya hayo, karibu kila

mtu kijijini kwao na katika ujirani alimuogopa na kumuheshimu pia. Sababu ni kuwa hakuwahi kumchokoza mtu hata mara moja. Kwa jumla alikuwa mpole na mtaratibu kama mwanakondoo ambapo hajakabiliwa na vita. Kutokana na nguvu hiza alizokuwa nazo. Mauti alijivuna sana ndani kwa ndani. Aliamini kuwa yeyote asiye na nguvu ni mtu alipokufa. Ungemsikia akisema, «kwa nini Fulani afe vivi hivi kijinga tu. Kwani hana nguvu za kupambana na kifo! Yeye ni mwanaume sampu gani !"

Kwa hakika, Mauti hakupata kulala hata siku moja kwamba alikuwa ameuguwa ama kuumwa hivi na vile. La hasha ungemsikia akisema kifo uko wapi? Njoo nikutwange ngumi.Nasikia una nguvu, kwani nini huji kwangu?

Watu waliozoea kusikia sauti hiyo ya bwana Mauti ikitishatisha kifo.Naam, angurumao simba mcheza nani?Si uongo. Kukutana anabwana Mauti wa Cheleamambo katika vita kulikuwa sawa kabisa na kukutana na mauti au kifo ana kwa ana.

Alfajili moja kulitokea shida. Samba dume wa kutisha alivaamia kijiji. Kufumba na kufumbua watu zaidi ya hamsini walilala fofofo wakiwa maiti vilio, mayowe na rabsha za kira namna ziltawala kijiji chote. Watu walijeruhiwa chungu nzima. Sahaulia mbali waliouawa kwa maneno makali ya samba huyo mkali. Walioparuzwa kucha hawakuwa na idadi.

Bwana Mauti sijui alikuwa wapi?Hadi alasili alikuwa hajaonekana wala maiti yake kupatikana. Alizuka kama mzuka wakati wa alasili huku jasho likimtiririka tiriri. Alilia kwa chungu alipoona jinsi wanzake walivyoshambuliwa na samba.

"Yuko wapi huyo mkorofi nipambane naye!" Mauti alisema kwa ukali.

"Ameingia kichakani kula mawindo yake!" Alijibiwa.

Na kweli samba alikuwa ameilaza tuli huku akitafuna minofu ya nyama za binadamu aliowaua. Mauti alikimbia kuelekea kichakani kwa mori kuliko chui. Wengine walisema kimoyomoyo «hata sisi tuna samba wetu!"

"Toka we shenzi!Toka nikuone!" Mauti alipayuka.

"Toka uko wapi?" simba hakujiyokeza.

Mauti alianza kuingia ndani ya kichaka.Alitaka amuone huyo simba anayesifiwa kuwa ndiye mnyama mwenye nguvu kuliko wote.

Mzee Guruguza alimtahadhalisha, “Twajua una nguvu usifanye mzaha mbele ya simba… Ondoka turudi nyumbani!”

Mauti alimtazama mzee Guruguzakwa jicho la dharau. Akafoka kwa ukali.

“Niache!Simba haniwezi.Nimewapiga wanye nguvu kuliko yeye.Nimewahi kupambana na mbogo nikamshinda sembuse simba asiekuwa na pembe!”

Akaingia ndani zaidi. Mara ngurumo kali kama radi ikasikika kutoka kichakani simba alipotokeza. Mauti aliona mauti wala hakumwona simba tena.

**Hatua ya 1 :** Soma hadithi hiyo tena upate kuielewa vilivyo.

**Hatua ya 2 :** Andika muhtasari wa mambo muhimu kama ifuatavyo :

1. Mzee Mauti aliishi katika kijiji cha Cheleamambo
2. Mzee Mauti alikuwa mkali na mwenye nguvu kabisa
3. Mzee Mauti alikuwa na majivuno kutokana na nguvu zake
4. Simba aliwaua watu wa kijiji cha Cheleamambo
5. Simba alimtoroka Mauti

**Hatua ya 3 :** Panga mambo ya muhtasari yafuatane kwa utaratibu

1. Mzee Mauti aliishi katika kijiji cha Cheleamambo
2. Mzee Mauti alikuwa mkali na mwenye nguvu kabisa
3. Mzee Mauti alikuwa na majivuno kutokana na nguvu zake
4. Simba aliwaua watu wa kijiji cha Cheleamambo
5. Simba alimtoroka Mauti

**Hatua ya 4 :** panua muhtasari kwa maneno yako mwenyewe

Mzee Mauti aliishi kijijini Cheleamambo. Alikua mtu mwenye nguvu pia mkali sana, alikua mzoefu wa kushinda vita. Watu wote walimuogopa, waliamini kuwa isipokuwa mauti huakuna yeyote yaweza kumshinda. Kwa hiyo alikuwa anajivuna sana. Siku moja kijiji kilishambuliwa na simba. Simba huyo aliwaua watu wengi. Mzee Mauti akasikitika sana

na akaamua kumuua simba huyo. Lakini kwa bahati mbaya simba akamtoroka. (**maneno 59**).

**Hatua ya 5 :** Andika nakala kamili ya ufupisho wako

Mauti

Mzee Mauti aliishi kijiji cha Cheleamambo. Alikuwa na nguvu tena mkali sana kutokana na uzoefu wake kushinda vita. Watu wengi walimuogopa na kudhani kwamba isipokuwa mauti, hakuna awezaye kumshinda. Kwa hiyo alikuwa mwenye majivuno sana. Simba akatokea kijijini kwao na kuwaua watu wengi. Mzee Mauti alijalibu kumtafuta simba ili amuue lakini akamkosa ghafla.

## MAZOEZI

Chagua jibu mufti :

1. Mzee Mauti alisifiwa kijijini kutokana na…………..
    a) Ukatili wake
    b) Wema wake
    c) Nguvu zake
    d) Upole wake
2. Maneno "sharti urambe ardhi"yalitumiwa kwa maana ya……………
    a) Lazima uanguke chini
    b) Hukanyagi ardhi
    c) Si lazima ufike chini
    d) Lazima ule udongo
3. Mtu anayeogofya husemwa…………………..na watu
    a) Anaogopewa
    b) Anaogopiwa

c) Anaogopwa

d) Aogopesha

4. Jambo la kushangaza ni kwamba Mauti…………….

   a) Aliugua mara kwa mara

   b) Hakuugua hata mara moja

   c) Aliogopa kifo pekee

   d) Aliskiia sauti ya mauti

5. Wanakijiji wachelea mambo siku moja…………

   a) Walishambuliwa na simba

   b) Walivamiwa na Mauti

   c) Walilala fofofo

   d) Walifaliki wote

6. Kukwangua au kutoa ngozi kwa kutumia kucha ni ……………

   a) Kugwara

   b) Kuchuna

   c) Kuparuza

   d) Kupora

7. Majeruhi ni ……………

   a) Watu waliopata majeraha

   b) Watu wanaowajeruhi wengine

   c) Watu walioumiza

   d) Watu wenye furaha

8. Waliolala fofofo katika habari hii ………………
    a) Walichoka
    b) Walikufa
    c) Waliumia
    d) Waliogopa

9. Jina linguine lililotumika hapa lenye maana sawa na simba ni …………
    a) Dume
    b) Nyamaume
    c) Chui
    d) Shenzi


10. Habari hii inatufunza kuwa …………
    a) Ni muhimu kupigana na simba
    b) Wanakijiji wa Cheleamambo ni woga
    c) Anayejivunia uwezo fulani humpata anayemzidi
    d) Mtoto wa nyoka ni nyoka

# SURA YA SABA : HOTUBA

## 7.1 Dhana ya hotuba

Hotuba ni maelezo maalum yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya watu kwa ajili ya kuwashirikisha, kuwaarifu kuhusu jambo Fulani, kuwaburudisha, n.k

Picha inayoonyesha mtu anayetoa hotuba mbele ya hadhira



## 7.2. Aina za hotuba

Kuna aina nne za hotuba : hotuba iliyotayalishwa kwa muswada, hotuba iliyokaliliwa, hotuba ya hapo hapo, hotuba ya papo kwa papo.

1. **Hotuba iliyotayarishwa kwa muswada** : hii ni aina ya hotuba ambayo husemwa kwa kutumia maneno yaliyotayalishwa kabla kusemwa mbele ya hadhira aina hii ya hotuba msemaji wa hotuba anajua atavyosema, ana matayalisho kwa mswada.
2. **Hotuba iliyokaririwa** : ni hotuba ambayo msemaji hukariri.
3. **Hotuba ya papo hapo** : ni hotuba inayotayarishwa kwa makini lakini msemaji husema bila kujiandaa au bila kutumia mswada. Msemaji hategemei miswada yake, hutegemea ujumbe anaotaja.
4. **Hotuba ya papo kwa papo** : ni aina ya hotuba isiyotayarishwa kabla ya kusemwa; husemwa bila maandalizi yoyote, hotuba hii mtu anaisema bila maandishi wala mpangilio wowote anatumia lugha ya mazungumzo. Aina hii ya hotuba haihitaji maandilizi wala mazoezi wala utafiti wowote.

Kufuatana na madhumuni ya hotuba kuna hotuba ya kushirikisha, hotuba kuarifu na hotuba ya kuburudisha.

a) **Hotuba ya kushirikisha :** ni hotuba ambayo inayowavuta na kuwahimiza watu kufuata mkondo Fulani, imani Fulani au mambo Fulani. Hotuba ya aina hii inawashirikisha watu, inawahimiza watu kufanya kama anavyofanya.

b) **Hotuba ya kuarifu** : ni aina ya hotuba yenye madhumuni ya kuarifu hadhira kuhusu jambo Fulani na kuapatia maarifa yanayohitajika kwao.

**c)** **Hotuba ya kuburudisha** : ni hotuba ambayo madhumuni yake ni kuburudisha hadhira.

## 7.3. MUUNDO WA HOTUBA

Hotuba inaundwa na sehemu kubwa tatu yaani **mwanzo**, **mwili** na **mwisho.**

**Mwanzo wa hotuba** ni muhimu sana kwa kuwa hadhira inampima msemaji katika sentensi za mwanzo; hadhira inaamua kuendelea kusikiliza au kuacha. Wanaamua kuwa mada ni muhimu au la.

Kuna kazi tano za mwanzo wa hotuba ambazo ni pamoja na kuwafanya watu wawe makini, kuonyesha umuhimu wa mada, kueleza lengo la hotuba, kujitambulisha na kuonyesha maendeleo na mpangilio wa hotuba.

**Mwili wa hotuba** ni sehemu kubwa ambayo inazingatia mambo muhimu kuhusu mada ya hotuba ambayo ni pamoja na mifano, maelezo, fikra na mambo mengine ambayo ni muhimu kwa kueleza mada hiyo.

Mwili wa hotuba huongeza ujuzi wa wasikilizaji kuhusu mada ya hotuba. Unabadilisha mwenendo wa hadhira, unafafanua kwa undani vidokezo vyote kwa kutumia mifano na maelezo vya kutosha, mwili wa hotuba huonyesha mahali ambapo vidokezo vilitoka.

**Mwisho wa hotuba** hutaja hitimisho ya yaliojadiliwa katika hotuba yote pamoja na mambo mengine muhimu ya msemaji, katika hitimisho msemaji anatayalisha wasikilizaji kuhusu mwisho wa hotuba yake msemaji huonyesha hadhira mahitaji yake kwao msemaji anamaliza hotuba yake kwa mbinu ya kuacha hadhira katika hamu ya kuendelea kusikiliza

## MFANO WAHOTUBA :

Bwana mwenyekiti wa kamati ya shule, Bibi mwenyekit i wa chama cha wazazi na wanafunzi wote hamjambo ?

Nimewaita nyote hivi leo wazazi na wa funzi wa dalasi hili la tano ili tuzungumze kwa mapana na marefu juu ya umuhimu wa ushilikiano baina yetu sote ikiwa tunataka maendeleo mazuri.Wahenga wasema upatilize udongo ungali maji.Ndiyo sikungonjea mwakani kuitisha mkutano. Hii ni safari ndefu na ngumu na msafiri ni aliyebandarini.

Madhumuni ya Kuwataka wazazi na wanafunzi ni kwa sababu matokeo mazuri yategemea, pamoja na walimu wangu wala siyo kutarajia shule kuwafanyia kila kitu, jiwe moja halitereki chungu .Kitu ambacho ningependa kusisitiza ni kwamba watoto wote ni sawa.Ha tuwezi kusema wa aina Fulani huzaliwa wajinga na wa aina nyingine huzaliwa welevu.Mungu hajapanga hivyo kwani hana tabia ya kupendelea wala ya kuonea.Swali linalotukabili ni : Kwa nini shule Fulani Fulani tu ndizo zenye matokeo mazuri mwaka nenda mwaka rudi? Jawabu ni kwamba wazazi hawawatendekezi watoto wao kama vile mnavyofanya wazazi wa shule hii.Kunradhini, leo, mambo ni ana kwa ana, hakuna kufichana.Wahenga husema : Ukistahi mke ndugu huzai naye.Hali kadhalika mnaambiwa : Ukicha mwakulia mwisho utalia wewe.

Ama kwa upande wa wanafunzi nawakumbusha kwamba, 'Mtaka cha mvunguni sharti ainame.'Matokeo yanataka ukakamavu, bidii, na kujitolea ndivyo wenzenu kama nyinyi wafanyavyo.'Ukiona vyaelea, vimeundwa'. Imani na matumaini makuu juu yenu.Sasa tutaketini shauri tushirikiane sote kwa dhati na sisi wenyewe tutaona yale ya kutufurahisha.

Nawashukuru kwa kunjisikiliza na naomba radhi kwa kosa lolote nililolisema kwani sikukusudia kumuudhi ye yote.

## MAZOEZI :

1. kufuatana na madhumuni ya hotuba taja aina za hotuba?
2. Fafanua sehemu tatu kubwa ya hotuba?

# SURA YA NANE : AINA ZA TUNGO

## 8.1. TUNGO

Tungo : Ni kipashio cha kimuundo kinachotokana na uwekaji pamoja wa vipashio sahili ili kujenga kipashio kikubwa zaidi yaani sentensi. Sentensi ni fungu la manenao ambalo lina kiima na kiarifu.

Katika Kiswahili tuna tungo ambazo ni fupi na zile ambazo ni pana zenye **kiima** na **kiarifu**.

***Kiima :*** Ni neno au ni kifungu cha maneno katika tungo ambacho hutangulia kitenzi na huonyesha mtenda.

***Kiarifu :*** Ni sehemu ya tungo ambayo huzungumza na hutoa habari juu ya kiima(A). Kiarifu ni kifungu cha maneno kama kitenzi, shamirisho, chagizo. Kiarifu huanza na kitenzi katika tungo.

**Mifano *:***

1. Msichana huyu amechelewa.
   K A
2. Mwalimu anasoma kitabu.
   K A

**Zoezi**

A. Onyesha kiima na kiarifu vya tungo zifuatazo.

   1. Juma anakula.
   2. Petro ana kalamu.
   3. Yeye halimi shamba.
   4. Timoteo na Jastini wanaandika barua.
   5. Dereva huyu anaendesha gari.

6. Mtumishi alifanya kazi kizee.
7. Wao hawapendi matata.
8. Kalisa na Afiya wanafanya kazi ya kuvua samaki ziwani.
9. Maria alianguka dharura shimoni.
10. Ng'ombe Yule mnene anakula nyasi ndefu mno.

B. Tunga tungo tanu fupi zenye muunodo wa kiima na kiarifu.

## 8.1.1. AINA ZA TUNGO

Kwa kawaida, Kiswahili kama lugha yoyote kina miundo ya tungo inayotofautiana. Kwa hiyo wanaisimu wameziainisha tungo za Kiswahili kutokana na miundo yake. Katika Kiswahili kuna miundo kama tano :

a. Tungo sahili
b. Tungo tegemezi
c. Tungo ambatano
d. Tungo changamano
e. Tungo shurtia

### 8.1.1.1. Tungo sahili

Tungo sahili ni tungo ambayo ni muundo wa fungu la maneno unaohusisha kirai-nomino na

kirai-kitenzi, na wenye maana kamili iliyokusudiwa. Kiini cha sentensi hizi ni kirai-kitenzi ambacho kwa kawaida huweza kutokea peke yake au kuandamana na vipashio vingine vya tungo kama virai nomino, virai vivumishi au virai vielezi.

**Mifano :**

1. Anatembea.
2. Juma anakula.
3. Maria ni msichana mzuri mno.

Kutokana na maana yanayoweza kujitokeza katika tungo sahili, tunaweza kapata tungo ambazo ni tungo Nyofu na tungo Tata.

*i.Tungo Nyofu*

Tungo nyofu ni ile ambayo ina maana moja kamili na yenye uwazi.

**Mifano :**

1. Kalisa anasema.
2. Mama yangu alinunua viazi mviringo.
3. Kamali anaandika daftarini.

Maana yanayojitokeza katika tungo hizi hapo juu ni ya moja kwa moja hayaleti utata.

*ii. Tungo tata*

Ni tungo ambayo inaweza kuwa na maana zaidi ya moja. Utata hutokea pale ambapo tungo huweza kueleweka hivi na vile na kila maana ikawa sahili. Kwa hiyo, maana nyingi zikamtatanisha mtu kujua tungo yenyewe inamaanisha nini.

**Mifano :**

1. Amemkanyaga motto.
2. Ameua simba.

Maana katika tungo ya kwanza yanaweza kumaanisha kuwa mtoto amekanyaga mtu fulani au mnyama fulani au mtoto amekanyagwa na mnyama.

## Zoezi

A. Tunga tungo tano sahili.

B. Miongoni mwa tungo zifuatazo bainisha zile zenye utata na zile zisizo na utata na utatue utata huo.

   1. Mwalimu Juma anakutafuta.
   2. Watoto wanacheza mpira.
   3. Aje Jumamosi.

4. Ali hali ndiyo maana hana hali.

5. Khamis anamsaidia mamake kupika chakula.

### 8.1.1.2 Tungo Tegemezi

Hii ni aina ya tungo ambayo haijitosherezi katika maana yake, yaani ni tungo ambayo ina hali ya kutegemea tungo sahili ili kuipa maana kamili.

**Mifano :**

1) Mtoto anayelia si mtoto wangu.

T.T T.S

2) Anaingia darasani ili afute ubao.

T.S T.T

### Zoezi

A. Bainisha tungo tegemezi katika sentensi zifuatazo.

1) Wakati atakapokuja nitaondoka.

2) Walikuwa wa kwanza waliofika saa moja.

3.) Anayebukua sana si mshindi.

### 8.1.1.3.Tungo Ambatano

Tungo ambatano ni tungo au sentensi ambayo ni kubwa humiliki tungo nyingine ndogo kwa kupitia kiunganishi kinachounganisha tungo hizo. Tungo ambatano ni tungo ambayo huundwa na tungo sahili zaidi ya moja.

Mifano :

1. Kaka yangu ameenda hospitalini kwa sababu ameumwa tumboni.

T.S U T.S

2. Rosa anaimba wimbo mzuri na anacheza ngoma.

T.S U T.S

**Zoezi**

A. Tunga tungo tatu zenye muundo wa tungo ambatano.

### 8.1.1.4. Tungo Changamano

Tungo changamano ni tungo ambayo huundwa na tungo sahili moja au zaidi ya moja na tungo tegemezi moja au zaidi. Sifa moja ya tungo changamano ni kuwa na tungo tegemezi ambayo hutegemea tungo zingine huru ndani ya sentensi hiyo.

**Mifano :**

1) Hakushtuka aliposikia mtoto wake analia.

T.S T.T T.S

2) Nitamuuliza atakayefika.

T.S T.T

3) Aliporudi nyumbani alitukuta tumelala.

T.T T.S

**Zoezi**

A.1. Kwa kutunga tungo tano changamano, bainisha ndani yake tungo tegemezi na tungo sahili.

### 8.1.1.5.Tungo Shurtia

Tungo shurtia ni sentensi yenye kitenzi ambacho hutoa taarifa kamili lakini usharti hutegemea sharti ya kitenzi hicho.

**Mifano :**

1. Ungefanya bidii ungefaulu mtihani.
2. Angelipelekwa hospitalini angelipona.

### Zoezi

**A.** Onyesha kitenzi kinachobeba shartio katika tungo zifuatazo.

1. Angemngonjea saa tatu angemuoana uso kwa uso.
2. Ungeweka rutuba shambani mwako ungepata mavuno ya kutosha.
3. Angelienda Marekani angelipata alama za kutosha.

# SURA YA TISA : SARUFI MIUNDO

## 9.1. UCHANGANUZI/UPAMBANUZI WA TUNGO

Tungo au sentensi ni kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo chenye maana kamili. Muundo wa sentensi hiyo huhusisha vipahsio viongine vidogo kimuundo. Katika Kiswahili muundo wa msingi wa sentensi huwa unahusisha virai tu na hasa kirai nomino na kirai kitenzi.

Muundo wa sentensi katika lugha huweza pia kuhusisha virai vingine kama vile virai vivumishi, virai vielezi na virai viunganishi. Kwa kawaida, virai vya aina hizi huwa hasa vina uamilifu wa kupanua maelezo ya virai nomino au virai vitenzi ndani ya sentensi.

**Mifano :**

1) Juma atampiga musa kesho asubuhi.

   KN KT

2) Maria anapenda kula matunda mara kwa mara.

   KN KT

3) KALISA na baba yake wanaenda kununua gari.

   KN KT

Uchanganuzi au upambanuzi wa tungo hutumia njia tatu yaani ***njia ya maneno, njia ya visanduku na njia ya matawi***.

### 9.1.1 Njia ya maneno

Upambanuzi wa tungo kwa kutumia njia hii huonyesha namna vipashio humiliki vipashio vingine kwa kutumia maneno.

| |
|---|
| Sentensi(S) ⟶ kirai nomino (KN) kirai kitenzi (KT) |

**Mfano :**

1. Juma anakimbia.

S ⟷ KN KT

(Juma anakimbia) (Juma) (anakimbia)

### 9.1.1.2. Njia ya visanduku

Hii ni njia ya kuchanganua sentensi kwa kutumia visanduku na kuonyesha kipashio ambamo kili nena linamilikiwa.

| S | | | |
|---|---|---|---|
| KN | | KT | |
| N | V | T | N |

**Mifano :**

1. Baba amenunua kitanda kikubwa.


| S | | | |
|---|---|---|---|
| KN | KT | | |
| N | T | KV | |
| | | N | V |
| Baba | amenunua | kitanda | kikubwa |

2. Wanafunzi wazuri wanasoma lugha.

| S | | | |
|---|---|---|---|
| KN | | KT | |
| N | V | T | N |
| Wanafunzi | wazuri | wanasoma | lugha |


### 9.1.1.3. Njia ya matawi

Katika sarufi miundo virai, kwa mwingine njia ya matawi ilibuniwa hasa kwa lengo la kuonyesha wazi jinsi vipashio vinavyomilikiana.





**Mifano :**


1. Juma anakimbia.




2. Baba amenunua kitanda kikubwa.



3. Kaka yangu amempiga mtoto wake fimbo.




### Zoezi

**A.** Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya visanduku na kwa njia ya matawi.

1. Kalisa anamtembelea Kamali.
2. Mtu mrefu ameondoka.
3. Mtoto amemletea mama yake kuni jana.
4. Kijana Yule mrefu alimnunulia mwana wangu soda jana asubuhi.
5. Mawike alipata faranga nyingi mno.
6. Mwalimu mwema anawasaidia wanafunzi.
7. Mama anapika chakula na Baba analala.
8. Amemletea gari nzuri.
9. Rais alisema hayo kwa amri ya jeshi.
10. Leo asubuhi, mwalimu aliwapatia wanafunzi wote alama zao za mitihani.

## MAELEZO YA VIFUPISHO

S : sentensi

KN : kirai nomino

KT : kirai kitenzi

KV : kirai kivumishi

KU : kirai kiunganishi

U : kiunganishi

V : kivumishi

N : nomino

E : kielezi

T : kitenzi

T.T : Tungo tegemezi

T.S : Tungo sahili

# SURA YA KUMI : UTUNGAJI

Barua (waraka) ni moja katika njia za mawasiliano ya siku hadi siku.Mtu mmoja humwandikia mwenzake huku akitegemea kupata majibu kwa yale aliyoyaandika.

Zipo aina mbili za barua : Barua za kirafiki (au za kindugu)

Na barua rasmi (au za kikazi).

## 10.1. BARUA ZA KIRAFIKI

Kuna madhumuni mengi yanayopelekea kuandika barua za kirafiki kama kusalimiana na rafiki zetu, kuwajulisha marafiki zetu maisha yetu ya kila siku, kuomba misaada wakati wa shida, kutoa shukrani baada ya kutendewa vyema au kutimiziwa maombi yetu, kutoa hongera, kutoa rambirambi, zetu kwa waliopatwa na msiba, na kadhalika.

**Barua za kirafiki zina sehemu muhimu zifuatazo :**

(a) Anuani ya mwandishi na tarehe

(b) Maamkizi

(c) Mwanzo wa barua

(d) Kiini cha barua

(e) Hitimisho na mwisho wa barua.

**(a) Anuani ya Mwandishi na Tarehe**

Anuani ya mwandishi huandikwa kwenye pembe ya juu, upande wa kulia wa karatasi. Katika barua za kirafiki, mpangilio wa mshazari hutumika sana kuandika anuani.

Kila mstali katika anuani huanza kwa herufi kubwa, na kumalizika kwa kutia alama ya mkato isipokua katika mstari wa mwisho ambapo baada ya jina la mji hutiwa kikomo/ kitone.

Iwapo vifupisho vitatumiwa katika anuani ni sharti mwandikaji atie kitone kila baada ya ufupisho.***Mfano :*** S.L.P badala ya Sanduku la Posita. S.L.P kwa maana ya Sanduku la

Barua haifai kwa sababu masanduku ya kukusanyia barua hupatikana hata mashuleni wala masanduku si masanduku ya posita.

Jina la mji huandikwa kwa herufi kubwa kwa jili ya kurahisisha utambuzi.

Kidesturi tarehe huandikwa chini ya mji kuanzia pale ulipoanzia mstari wa kwanza wa anuani.Kwa kuwa barua huhifadhiwa tarehe inahitajika kwa madhumuni ya kuweka kumbukumbu na barua huweza kurejelewa katika siku za usoni.

**Angalizo :** Mwandishi asiandike jina lake pamoja na jina na anuani yake. Majina ya mwandishi wa barua huandikwa mwishoni kabisa mwa barua.

**Mpangilio wa mshazari**

Shule ya Upili Buhuga,

S.L.P.123,

MUSANZE.

Agosti 14, 2000.

Inakubalika pia kutumia mikwaju14/8/2000, vitone : (14.8.2000), au visitari (14-8-2000)

**Mpangilio wima :** Anuani ya mwandishi katika barua ya kirafiki huweza pia kuandikwa kwa mpangilio wima kama hivi ifuatavyo :

Shule ya Upili ya Buhuga

S.L.P, 123,

USANZE.

Agosti, 14, 2000.

**(b) Maamkizi**

Baada ya kuandika anuani, inampasa anayeandika kuruka msitari mmoja na kisha kuanzia kwenye pambizo la kushoto la kalatasi kuandika maamkizi.Maamkizi hutegemea uhusiano baina ya anayeandika na anayeandikiwa.

**Mifano :**

Mpendwa Baba**,**

MpendwaKaka,

Rafiki Mpenzi naMwanangu Mpenzi.

Kila herufi ya kwanza katika kila neno lililomo katika kila maamkizi au kianzio kama vile**"M"** katika'Mpendwa' na "**B**" katika'Baba′ inapasa ziwe herufi kubwa.Mwishoni mwa maamkizi mwandishi sharti atie alama ya mkato kama ilivyo katika mifano hapo juu.

**(c) Mwanzo wa barua**

Kwa kawaida, barua ya kidugu huanzia kwa salamu na kumjulia hali anayetumiwa barua .Salamu nazo hutegemea uhusiano baina ya mwandishi wa barua na mwandikiwa.Kwa mfano iwapo mwandikiwa anamzidi mwandishi umri, anaweza kuanza kwa kuamkia; Shikamoo!

**(d) Kiini cha barua**

Mwanzo wa aya mpya huanzia kwa herufi kubwa kwenye msitari unaofuatia, chini ya alama ya mkato.Barua za kirafiki kwa kawaida huanza kwa salamu au kujuliana hali.

Barua za kidugu hutumia lugha ya kawaida isiyo na urasmi, lakini inatakikana iwe lugha yenye adabu na yenye heshima.Pia itategemea sana uhusiano baina ya anayeandika na anayeandikiwa.Kwa mfano lugha ya barua kwa mzazi itakua tofauti na barua kwa mtani wa mwandishi.

Maneno yote yanayoptumiwa yapewe mazingatio kwa kuwa mara kwa mara barua huhifadhiwa na kuweza kurejeelewa baadaye.Hivyo basi barua ziandikwe kwa makini nakituo.

Mwandishi aandike kamakwamba anazungumza ana kwa ana na mwandikiwa.Ni muhimu igawanywe katika aya na kila jambo jipya liandikwe kwenye aya mpya.Barua za kimtihani ziwe na urefu uliopendekezwa na zibebe maudhui sita.Mwandikaji atumie mwandiko ulio nadhifu.

**(e) Hitimisho na mwisho wa barua**

Barua ihitimishwe kwa maneno ya kuvutia.Barua hizi za kidugu humalizika kama vile :

Wako mpendwa,

Ndimi kakako mpendwa,

Ni mimi mwanao

Wako wa moyoni,

Wenu,

Rafikiyo akupendaye, kulingana na uhusiano baina ya mwandishi na mwandikiwa.

Maneno ya kuhitimisha yaanzie katikati mwa mstari kuelekea upande wa kulia wa karatasi. Herufi ya kwanza katika mstari huo kama vile "**W**" katika 'Wako' inafaa kuwa herufi kubwa.Herufi za kwanza katika maneno yanayofuata kama vile "**m**" katika mpendwa, huwa ni herufi ndogo.

Hatimaye mwandikaji wa barua aandike majina yake kamili.

## KIELELEZO CHABARUA YA KIRAFIKI

Chuo Kikuu Cha Ualimu Cha Kigali

S.L.P.5039,
KIGALI,
Rwanda.
4 Mei, 2002

Mama Mpendwa,

Shikamoo!

Asante sana kwa barua yako ya tarehe 3 Aprili 2002.Nina furaha kusikia kwamba hamjambo nyote huko nyumbani. Je, Baba pia hajambo? Namsalimu sana.

Mimi huku pamoja na wanafunzi wenzangu hatujambo.Hatuna shida yoyote isipokuwa masomo magumu yanayotukabili muhula huu.sPia, tunashughulika na michezo mbalimbali kama vile riadha na kandanda. Tunatarajia kufunga masomo yetu ya mhula huu mwishoni mwa mwezi huu.Mara tu tutakaporuhusiwa kwenda likizoni nitakuja moja kwa moja huko nyumbani ili niwe nanyi tena, pamoja na kuwasaidieni katika kazi za shambani.Nisalimie wote huko nyumbani.

Mwanao mpenzi
Sophie MUKAMANA

## MAZOEZI (A)

1. Eleza sehemu kuu za barua ya kirafiki.
2. Onyesha muundo wa barua ya kilafiki.
3. Tofautisha mpangilio wa mshazari na mpangilio wima.

## MAZOEZI (B)

**a)** Una rafiki yako huko Malekani ambaye ametia nia kuja kuzuru hapa Rwanda. Mwandikie barua ukimweleza kuhusu vivutio vya kitalii vilivyopo nchini.

**b)** Rafi yako anayesoma katika kidato cha nne amefukuzwa shuleni kwa sababu ametumia dawa za kulevya na kushiliki ulevi.Mwandikie barua ukimshauri kuhusu hali hiyo na kumuonya.

**c**) Hivi karibuni ulikuwa miongoni mwa wanafunzi wa shule yenu walioshiliki katika mashindano ya michezo ya kuigiza, Mashairi na ngoma za kiasili.Andika barua kwa shangazi yako ukimsimulia mambo yalivyokuwa.

## 10.2.BARUA RASMI(Barua za Kikazi)

Barua za kikazi ni za aina nyingi, kwa mfano :

- Barua za maombi ya nafasi za masomo,
- Barua za maombi ya nafasi za ajira(kazi)
- Barua kwa wahariri wa magazeti
- Barua za mialiko rasmi,
- Barua za malalamishi na barua za kouomba radhi.

Barua rasmi zina kanuni na misingi maalum inayolazimu kuzingatiwa.Zifuatazo ndizo sehemu muhimu za barua rasmi :

✓ Anuani ya mwandishi na tarehe.

✓ Anuani ya mwandikiwa.

✓ Maamkizi.

✓ Mtajo (kichwa cha barua).

✓ Hitimisho na mwisho wa barua.

### (a) Anuani ya Mwandishi na Tarehe

Anuani ya mwandishi huandikwa kwenye pembe ya juu ya karatasi upande wa kulia, katika mpangilio wima.Kila mstari unapashwa uanze na herufi kubwa na umalizike kwa alama ya mkato, isipokuwa mstari wa mwisho unaotaja jina la mji na baada mwaka katika tarehe ambapo hutiwa kikomo.Jina la mji liandikwe kwa herufi kubwa, kwa ajili ya utambuzi wa haraka.

Tarehe huandikwa chini ya jina la mji.

**Mfano :**

Kampuni yaUvuvi wa Gashora,

S.L.P.456 KIGALI.

Aprili 6, 2000.

**Angalizo :** Majina ya mwandishi yasiandikwe pamoja na anuani.

### (b) Anuani ya mwandikiwa(Mtumiwaji)

Anuani ya mwandikiwa huandikwa baada ya kuruka mstari mmoja toka kwa anuani ya mwandishi.

Anuani hii iandikwe upande wa kushoto kuanzia kwenye pampizo la karatasi, kwa mpangilio wima.Mwandishi wa barua aanze kwa kuandika jina au cheo cha mwandikiwa;kutegemea aina ya barua rasmki kama hivi :

(Isomeke : Imwendee)

Shilika la Posita na Simu,

S.L.P, 789,

KIGALI.

Barua rasmi hutumiwa moja kwa moja imwendee mtumiwaji mwingine lakini wakati mwingine kwa sababu ya urasmi uliopo katika taratibu za kiofisi, inalazimu barua rasmi imupitie au iwapitie maofisa wa ngazi Fulani za uongozi na utawala au wadhamini kabla ya kumfikia mlengwa.Katika hali kama hiyo, baada ya anuani ya mwandikiwa, mwandikishi wa barua huruka mstari mmoja na kuandika maneno : **Impitiee** au **Kupitia kwa** na kisha akaruka mstari mwingine na kuandika anuani ya afisa ambaye barua inampitia.

**Mfano :**

Kupitia kwa :

Mkuu wa mkoa,

S.L.P, 901,

MUSANZE.

Au

Impitiee :

Mkuu wa Mkoa,

S.L.P.901,

MUSANZE.

Iwapo kuna namba ya kumbukumbu (ya rejea) ya barua, basi namba hiyo huandikwa kwenye pembe ya kushoto ya juu ya karatasi.

### (c) Maamkizi

Mwandishi wa barua aruke mstari baada ya kuandika anuani ya mwandikiwa aandike maamkizi kuanzia kwenye pambizo la karatasi.Lugha rasmi itumiwe katika kuandika maamkizi.

**Mfano :**

Bwana, au

Mabwana, au

Mabibi na Bwana

Inampasha atie alama ya mkato baada ya maamkizi .Katika barua rasmi, ya" Mpendwa Afisa wa Uajili", Mpendwa Meneja, haipasi kutumika wala mwandishi hahitaji kumsabahi anayeandikiwa.

### (d) Mtajo

Kuanzia kwenye pambizo la karatasi, mwandishi huandika mtajo kwa kutumia herufi kubwa.Mtajo hudokeza kwa ufupi kuhusu madhumuni au mada kuu ya barua.Kichwa katika hutanguliwa na vifupisho vya kuonyesha madhumuni yenyewe.Baadhi ya vifupisho vinavyotumika ni hivi vifuatavyo :

KUH : Kuhusu au Kuhusiana na

MINT : Mintirafu

YAH : Yahusiana na

TAZ : Tazama

REJ : Rejeo

Vifpisho hivi vinapasha kuandikwa herufi ndogo na kufuatiwa na nukuta mbili ili kuonyesha kwamba kuna maelezo yanayofuatia.Maelezo ya mtajo huandikwa kwa herufi moja fupi naq kupigiwa mstari.

### (e) Maudhui

Maudhui ya barua rasmi hutofautiana na nia ya barua hiyo.Tunasisitiza kuwa barua za kimtihani ziwe za urefu unaotakikana.Katika barua rasmi mwandishi hayuko huru kuandika jambo lolote apendalo. Kwa hivyo utani na mizaha huwekwa pembeni .Inapasa barua rasmi iandikwe kwa nadhifu ya mkono yanayosomeka vizuri.

Aidha inatalajiwa iwe na aya mbalimbali .Kila mada mpya iandikwe katika kila aya mpya kwa mtindo wa moja kwa moja.Mwandishi aruke mstari kila baada ya aya .Aya zote zianzie kwenye pambizo la karatasi.

### (f) Hitimisho

Barua rasmi huhitimishwa kwa maneno kama vile :

Wako mwaminifu,

Wako mtiifu,

Wenu watiifu,

Herufi ya kwanza "W"katika 'Wako' iwe herufi kubwa na "m" mwanzoni mwa 'mtiifu' na' mwaminifu 'ziwe ndogo.Maneno hayo yaanzie pambizoni kuelekea kulia.Kisha mwandikishi atie saini ili kuwekea barua yake uzito na hatimaye aandike majina yake kamili kwa herufi kubwa.

Chini ya majina waandishi waandike vyeo walivyo na vyo kwa herufi kubwa kama inalazimu.Kutokana na utaratibu wa kikazi, wakati mwingine hupelekewa nakala za barua rasmi :

**Mfano :**

Nakala kwa :

Meya wa Gakenke,

S.L.P.200,

MUSANZE.

Maelezo ya anuani za walionakiliwa barua huandikwa baada ya kuhitimisha barua na jina la mwandishi wa barua.

## 10.3.BARUA YA KIKAZI

Shule ya Msingi ya Cyintare

S.L.P.12,

MUSANZE,

Rwanda.

Oktoba14, 2000.

Kumb No. KB/4/2002

Afisa Elimu,

S.L.P .164,

MUSANZE,

Rwanda.

Bwana,

**KUH : Maombi ya Kazi ya Ualimu**

Ninayo heshima kuomba kazi ya Ualimu katika shule ya Msingi ya Cyintare wilayani Gakenke.Mimi nilisomea katika Chuo Kikuu Cha Ualimu Cha Kigali nikahitimu kama mwalimu wa kufuzu.

Mimi ni Mnyarwanda, nina miaka thelathini na minne na sijaoa bado.Ninaweza kufundisha Kiswahili, Kingereza, na Historia. Pia, ninapendelea michezo na kazi za mikono.

Nitashukuru sana iwapo ombi langu litafikiriwa na kupokelewa vyema.

Wako mtiifu,

Anastase ICYOYISHAKIYE,

MWALIMU

## MAZOEZI (A) :

1. Onyesha muundo wa barua ya kikazi.
2. Toa tofauti iliyoko kati ya barua ya Kirafiki na ile ya Kikazi

## MAZOEZI (B) :

Tangazo lifuatalo lilitokea katika gazeti la Imvaho Nsha hivi karibuni.

Halmashauri ya Rwanda inakaribisha maombi ya kazi kutoka Wanyarwanda wenye sifa timilifu kwa ajili ya nafasi ifuatayo ya kazi .

**MENEJA**

**Sifa za waombaji :**

i) Wawe na angalau Shahada za chuo Kikuu katika biashara au sifa zote zinazofanana na hizo.

ii) Wawe na utaalamu na tajriba katika nafasi kama hiyo isiyopungua miaka mitano.

iii) Wawe na umri wa miaka isiyopungua thelathini na mitano.

Maombi ya kazi yakiambatana na majina mawili ya wadhamini yatumwe kwa :

Afisa wa uajiri

Halmashauri ya Kahawa ya Rwanda,

S.L.P, 5080,

KIGALI.

## 10.4. BARUA ZA KIBIASHARA

Kimuundo haina tofaouti na barua ya Kikazi.Mpangilio ni ule ule.Tofauti zenyewe zinaweza kujitokeza katika ujumbe.Barua za Kikazi ujumbe unalenga maombi wakati madhumuni ya barua za kibiashara yanahusu maagizo .Katika barua za Kibiashara hakuna sababu za kueleza uwezo.Ni kwa unahitaji vitu unavyoagiza au unavyoulizia hali au bei yake. Lugha inayotumiwa katika barua za Kibiashara, siyo ya kiofisi.Ikiwa ni mfanya biashara anamtumia ujumbe mteja wake ni lazima lugha yake iwe ya kuvutia wateja.

MFANO WA BARUA YA KIBIASHARA

Kumb.na.vm/16/82

Shule ya Sekondari

Rwanda

S.L.P.15,

RWANDA

Tarehe : 8/1/2011

Meneja,

Duka la vitabu

S.L.P, 606, KIGALI.

Bwana,

*KUH : VIFAA VYA SHULE*

*Tafadhali tuna vifaa vifuatavyo kwa ajili ya matumizi ya shule.*

i) *Madaftari tano mia(500)*

ii) *Matufe matatu(3)*

iii) *Rula za ubaoni kumi (10)*

iv) *Chaki nyeupe makasha ishirini (20)*

v) *Chaki za rangi makasha tano (5)*

vi) *Mipra ya miguu dazani moja.*

*Pamoja na orodha hii ya vifaa pokea kundi faranga elfu themanini na tano(85, 000)zikiwa ni malipo ya vifaa vyote hivyo.*

*Mkuu wa shule*

*Alexandre DUSHIMIRIMANA*

## 10.5.BARUA YA GAZETINI

Katika barua za gazetini mambo yafuatayo ni muhimu :

i) Anuani ya jina sahili la mwandishi hivi huandikwa chini ya ujumbe wa barua mkono wa kulia.

ii) Urefu wa barua za gazetini huwa fupi.Kwa kuwa ni mambo muhimu tu yanayoandikwa.

iii) Barua hizo hutumwa kwa mahariri.

iv) Mtu anayeandika barua ya gazetini lazima awe na hakika kwa kituanachoandika.

### MFANO WA BARUA ZA GAZETINI

**Ujambazi NYAGASANGE**

Mhariri,

NYAGASENGE ni sehemu inayopakana na nchi ya Uganda panakutania watu wengi toka Rwanda na Uganda .Jambo la kutisha na kutatiza sana ni kuwa ujambazi na ukahaba huongezeka usiku kucha, sehemu hii ina hali mbaya sana.watu sita waliua jana na wengi wamejeruhiwa na majambazi . Kutokana na ukosefu wa usarama watu wengi wana wasi wasi hasa hasa jioni kwa kuwa polisi hawapatikani kwa urahisi. Mara nyingi vitendo viovu husababisha vifo na ghasia hehemu hiyo.

Kutokana na hali hii tunaiomba selikali yetu ifikirie namna ya kulinda usarama eneo hili.

DUSHIMIMANA Eduard

S.L.P, 27 Kigali

## MAREJEO


- Ndalu, A.(1997). *Mwangaza wa Kiswahili*, E.A.E.P Limited : Nairobi.
- TUKI. (2004/2002/1993/1985). Fasihi simulizi : Vitendawili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam : Dar es Salaam.
- Ngure, A.(2007/2006/2005/2004/2003). *Fasihi simulizi kwa shule zasekondari,* Phoenix Publishers : Nairobi.
- TUKI. (2004/2002/1993/1981). *Fasihi Simulizi : Methali :* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam : Dar es Salaam.
- Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari. (1987). *Kitabu cha KiswahiliIV-VC* : *Kitabu cha Mwanafunzi*, Regie de l'Imprimerie Scolaire : Kigali .
- Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B., Msanjila, Y.P.(2008/2007/2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) : Sekondari na Vyuo,* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam : Dar es Salaam.
- MASSAMBA, D.P.B, KIHORE, Y.M, Hokororo, J.I(2001/1999*). SarufiMiundo ya Kiswahili Sanifu(SAMIKISA) : Sekondari na Vyuo*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam : Dar es Salaam
- RWABUSHAIJA, M.(2002). *Masomo ya msingi wa Kiswahili*, Fountain Publishers : Kampala.
- Bakhressa Salim, K.&Islam K.(1999/1998/1997/1996/1995). *Kiswahili Sanifu : Darasa la saba,* Oxford University Press : Oxford New York.
- Mbunda, M.(1993). *Misingi ya uhakiki wa Fasihi*, English Press Limited : Nairobi.
- DIETSCH, B.M(2003/2000/1998*). Reasoning& writing well*, M C Graw Hill Companies : New York.
- Pearson, J, C& Nelson, P.E&Titsworth, S.&Horter, L.(2003). *Human communication*, MC Graw Hill Companies.
- TUKI. (2003). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam : Dar es Salaam